ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake

52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

53.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

55.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

57.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

58. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

62.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

63.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

65.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

66.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

67.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

68.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

69.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndg. Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 20 Aprili, 2012

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 115

Uchakavu wa Barabara

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza**:-**

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekua ikichukua hatua ya kuimarisha miundombinu ili kuharakisha maendeleo kwa wananchi wake.

(a) Je, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ina mpango gani wa kujenga barabara ya Kibigija – Mfumbwi ambayo inakabiliwa na uchakavu mkubwa na kuwa kero kwa wananchi.

(b) Mhe. Waziri, kwa vile wananchi wamekuwa na kilio cha muda mrefu juu ya tatizo hilo. Je, ni lini Wizara inatarajia kumaliza kilio cha wananchi hao.

(c) Je, Mhe. Waziri, unatoa ahadi gani kwa wananchi kupitia Baraza hili tukufu la Wawakilishi kuhusu tatizo hilo huku ukijua kwamba utalii unakua katika kijiji cha Jambiani.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 116 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo lakini kabla ya kujibu naomba kutoa maelezo mafupi:-

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekua ikichukua hatua mbali mbali za kuzijenga na kuzitunza barabara kuu vijijini na mijini *(trunk, rural, urban and feeder roads)* katika maeneo mbali mbali ya visiwa vya Unguja na Pemba ili kuwarahisishia wananchi katika huduma za usafiri pamoja na mizigo yao kutoka sehemu moja hadi nyengine. Miongoni mwa barabara zilizojengwa kwa kiwango cha lami ni barabara ya Makunduchi ambayo imepitia katika eneo la Jambiani.

Baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Serikali kwa muda huu haina mpango wa kuijenga barabara ya Kibigija – Mfumbwi kwa kiwango cha lami kwa vile tayari vijiji hivyo pamoja na Paje, Michamvi, Makunduchi, Bwejuu na Jambiani yenyewe hadi Makunduchi barabara ya Kigaeni vimeshapata mradi mkubwa wa barabara ya lami.

(b+c) Mhe. Spika, kama kuna suala la kuimarisha barabara hiyo kwa kiwango cha kifusi ya kutoka Jambiani Kibigija – Jambiani Mfumbwi naomba tuendelee kushirikiana kwa karibu kati ya idara yetu ya *UUB*, Halmashauri ya Wilaya ya Kusini pamoja na viongozi wa Jimbo la Muyuni.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu ya kuwavunja moyo wananchi wa Jimbo la Muyuni hasa kijiji cha Jambiani naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kijiji cha Jambiani ni eneo moja linalochangia pato la taifa kupitia utalii.

(a) Je, Mhe. Waziri kutotengeneza barabara ile huoni kwamba unarudisha nyuma maendeleo ya wananchi wa Jambiani.

(b) Kwa kua suala la kupata huduma kwa wananchi ikiwemo miundombinu ya barabara ni haki ya kikatiba. Je, serikali ina mpango gani wa kujenga barabara ikizingatia vipi haki za katiba kuwapa wananchi huduma vile vile ikiwa wewe ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano itaendelea kutetea sera na kauli mbiu yake ya kuimarisha barabara kubwa mijini na vijijini. Tutaendelea kusema kauli yetu kwamba barabara hizi za ndani bado litaendelea kuwa jukumu la halmashauri zetu. Wajibu wetu ni kuwasaidia halmashauri pamoja na viongozi wa maeneo husika kusaidiana na idara yetu ya UUB katika kufanikisha miradi kama hii.

Mhe. Spika, imani yangu kwamba wananchi wa Muyuni wakiwemo wananchi wa Jambiani hawatovunjika moyo kwa kutojengwa barabara hii. Kama tunavyotambua kuna mradi mkubwa wa barabara ambayo imetoka Paje – Makunduchi Kigaeni ni barabara ya lami na ninaamini wananchi wa Jambiani wanaipongeza sana serikali yao kwa hatua iliyofikia.

Mhe. Spika, ombi langu kwa Mhe. Mwakilishi kwamba kama kuna ulazima wa barabara hiyo ya ndani basi namuomba tu aendelee kuimarisha ushirikiano kati yake yeye mwenyewe binafsi, viongozi wenzake wa jimbo, Halmashauri ya Wilaya ya Kusini na idara yetu ya *UUB*, ili kwenda kuwaona wananchi wakiweza kuwapatia vitendea kazi idara yetu ya *UUB* itawasaidia wananchi katika hiyo njia ya ndani. Lakini kwa jukumu la wizara hatuna mpango wa kujenga barabara ya lami katika eneo la Jambiani Kibigija – Mfumbwi.

Mhe. Spika, jibu (b) sidhani kwamba kutojenga barabara hiyo tutakuwa kama wizara tumekiuka majukumu yetu kwa mujibu wa katiba. Kwa sababu msingi wa kupeleka maendeleo ya wananchi tumeshautimiza katika mradi ule mkubwa wa barabara iliyotoka Paje – Makunduchi Kigaeni.

Nam. 116

Kuzuia Vyombo vya Moto vya Mitumba

Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa.

Nam. 125

Elimu ya Cheti katika Vyuo vya Ualimu Nchini

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa – Aliuliza:-

Kwa muda sasa Serikali iliondosha elimu ya cheti kwa walimu wa Zanzibar kwa lengo la kuanza kutoa diploma na digrii ya Ualimu, huku ikichukua hatua za kuajiri walimu waliosoma diploma na digrii.

(a) Mhe. Waziri, huoni kwamba uamuzi wa Serikali wa kuachana na walimu wa cheti unachangia kuongezeka kwa vijana wasio na ajira nchini.

(b) Je, kwa miaka ijayo, wanafunzi wa chekechea na madarasa ya awali ya msingi (kuanzia darasa la kwanza hadi la nne) watapata wapi walimu wenye uwezo wa kufundisha ngazi hiyo ya elimu.

(c) Kwa kuzingatia umuhimu wa elimu ya msingi na chekechea. Mhe. Waziri, utakubaliana na mimi kwamba umefika wakati wa kurudisha elimu ya cheti kwa vyuo vyetu vinavyotoa elimu ya Ualimu nchini.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 125 lenye sehemu (a), (b) na (c).

Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo. Ni kweli kwamba mafunzo ya cheti cha ualimu yanayotahiniwa na Baraza la Mitihani Tanzania yalisitishwa kutokana na kuwepo kwa wahitimu wengi ambao hawajaajiriwa. Mafunzo ya cheti cha elimu mjumuisho hayakusitishwa na yanaendelea hadi hivi sasa kutokana na kuwepo mahitaji makubwa kwa walimu wa aina hiyo ambao hutoa elimu na huduma kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum walioko katika skuli zetu. Vile vile mafunzo ya cheti cha ualimu kwa njia ya elimu masafa yanaendelea kutolewa kwa walimu walioko kazini.

Aidha, Wizara imeanzisha stashahada ya ualimu wa msingi ili walimu wanaofundisha madarasa ya msingi nao wawe na uwezo mkubwa wa kielimu na hivyo kutoa elimu iliyo bora zaidi. Tokea kuanzishwa kwa kozi hiyo ya stashahada ya ualimu wa msingi, vijana wengi wamejiunga na mafunzo ya ualimu katika ngazi hii na baadae kufundisha katika skuli za msingi. Baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali lake Nam. 125 (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

a) Wizara kusitisha kutoa mafunzo ya cheti cha ualimu hakuna uhusiano kabisa na kuongezeka kwa vijana wasio na ajira kwa sababu uajiri hutegemea kuwepo kwa nafasi tupu ya kazi na wala sio kuwaajiri wahitimu hata kama nafasi ya kazi hakuna. Hivi sasa idadi ya walimu ambao wameshahitimu mafunzo ni wengi kuliko mahitaji ya skuli zetu na matokeo yake baadhi ya wahitimu hawajaajiriwa hadi hii leo. Hivi sasa wapo wahitimu wa mafunzo ya ualimu zaidi ya 4,500 wanaohitaji kazi ya ualimu.

b) Wizara yangu ikishirikiana na Chuo cha Elimu cha Aga Khan huko Dar-es- Salaam, hivi sasa inaandaa kozi ya kutayarisha wakufunzi wa elimu ya maandalizi. Kozi hiyo itawatayarisha wakufunzi 25 Unguja na Pemba ili nao waje kutoa mafunzo kwa walimu watakaofundisha elimu ya maandalizi. Pia Wizara ikishirikiana na Shirika la Maendeleo la Sweden *(SIDA)* inakusudia kusomesha katika Vyuo vya Tanzania Bara katika ngazi ya stashahada na shahada wakufunzi watakaobobea katika elimu ya maandalizi. Wakufunzi hao watatumika katika kuandaa mafunzo ya walimu wa maandalizi katika vyuo vyetu vya ualimu na kupitia vituo vya walimu vya Saateni (Unguja) na Chachani (Pemba).

   Aidha, Wizara inakusudia kutoa mafunzo ya cheti kwa walimu wa maandalizi kwa kutumia teknolojia za kisasa. Walimu watasoma kwa kupitia *electronic modules* pamoja na *radio program.* Ni mafunzo ya miaka miwili na yatafanyika kwa njia ya elimu masafa *(open and distance learning).* Walimu watakua wakikutana na wakufunzi wao katika vituo vya walimu kwa mazoezi ya vitendo na nadharia. Mafunzo hayo yote yatamuwezesha mwalimu kufundisha madarasa ya maandalizi ya awali na msingi.

c) Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema, wizara inakusudia kuanzisha mafunzo ya cheti cha Ualimu wa maandalizi na awali msingi. Hivyo mafunzo ya namna hiyo yataanzishwa kutokana na mahitaji yaliyopo. Hata hivyo, napenda kusisitiza kuwa nia na azma ya Wizara kuhakikisha kuwa walimu wote wanakuwa na elimu isio chini ya kiwango cha stashahada.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Mhe. Spika, nakushukuru kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Je, Mhe. Waziri, hawa walimu wa cheti waliobakia ni wangapi hawajaajiriwa na lini wataajiriwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu mama kua hivi sasa tuna walimu karibu 4,500 ambao hawajaajiriwa. Kati ya hao kuna walimu 2,000 wa ngazi ya cheti ambao bado hatujawaajiri. Walimu hao Mhe. Spika, tutawaajiri tu pindipo tutakapopata ruhusa ya kuajiri. Mhe. Spika na Baraza lako tukufu, mnakumbuka kama tuliomba walimu 800 kwenye bajeti yetu. Kati ya walimu hao 800 tulikusudia angalau tupunguze hao walimu wa cheti. Kwa hivyo, kila tutakapopata nafasi ya kuajiri basi hawa tutawapunguza kidogo kidogo mpaka watamalizika.

Mhe. Nassor Ali Salim: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, ili mwalimu aweze kujiunga na diploma ya msingi au ya sekondari. Ni sifa gani zinazohitajika ili walimu wetu tuweze kuwahimiza kujiunga na kukuza elimu yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, sifa ya kwanza ambayo unatakiwa kujiunga na diploma ya msingi lazima uwe umesomea cheti hicho cha ualimu ambacho tulikuwa tukikizungumza. Lakini pia uwe angalau una uzoefu wa miaka mitatu katika kufundisha kwenye skuli zetu. Lakini pia uwe umepasi masomo matatu katika *'O' level.* Mhe. Spika, sifa ya kujiunga na diploma ya sekondari uwe umemaliza kidato cha sita. Hivi sasa tuna madarasa ya kidato cha sita karibu 21, sasa wale wanafunzi wetu ambao hawabahatiki kuingia katika chuo kikuu basi hao huwa tunawachukua kwa mafunzo ya ualimu na hao huwa wanakubalika kuchukua diploma ya sekondari.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, walimu 4,500 ni wengi na hawajaajiriwa na hapa petu kuna skuli nyingi za watu binafsi.

(a) Je, wizara imefanya utaratibu gani kuzungumza na wamiliki wa skuli za binafsi ili kusaidia tatizo hili.

(b) Kwa kuwa walimu 4,500 kusomeshwa na serikali ni gharama kubwa. Je, haoni kwamba walimu hao kutoajiriwa ni hasara kwa serikali.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, hawa walimu 4,500 ambao niliwazungumza hapa tayari tumeshazungumza na skuli binafsi na tayari wameshachukua walimu wetu. Mara nyingi skuli binafsi walimu ambao wanaajiri basi ni hawa walimu ambao tunazalisha sisi hawana sehemu nyengine za kuchukua walimu. Wengi wao labda ambao ni walimu wachache huchukua Kenya na Uganda lakini asilimia kubwa ni hawa walimu ambao tunawasomesha sisi Zanzibar.

Mhe. Spika, niseme Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali sifa yake moja ni kusomesha kujenga msingi wa mwanafunzi, tukishamsomesha ajira anaweza akatafuta popote. Mimi sioni kama kutokuwaajiri hawa 4,500 ni hasara kwa sababu tayari tumeshawajengea mazingira mazuri ya ajira, kama hatutowaajiri sisi basi wataajiriwa na sekta binafsi.

Nam. 126

Wanafunzi wa Zanzibar kupata Mikopo ya Kusoma nje ya Tanzania

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa - Aliuliza**:-**

Kwa muda mrefu sasa ofisa aliyekuwa anashughulikia mikopo ya Elimu ya Juu inayotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa upande wa Zanzibar amestaafu wakati bado hajachaguliwa ofisa mwengine kushika nafasi hiyo ili kutekeleza majukumu yaliyoachwa.

(a) Je, Serikali haioni kwamba kitendo hicho kinainyima Zanzibar nafasi yake ya kuwa na wanafunzi wanaopewa mikopo ya kusoma vyuo vilivyo nje ya Tanzania.

(b) Kwa kipindi chote hicho tokea kustaafu kwa ofisa huyo. Je, ni wanafunzi wangapi wa Zanzibar wamepata mikopo ya kusoma nje ya Tanzania.

(c) Je, ni lini Serikali itahakikisha kwamba nafasi hiyo ya ofisa inajazwa kwa kuwakilishwa na ofisa mwengine atakayesimamia maslahi ya Wazanzibari.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 126 lenye sehemu (a), (b) na (c). Kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:

Ni kweli kuwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa mikopo kwa wanafunzi wanaojiunga na Vyuo vya Elimu ya Juu, kutoka sehemu zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Serikali ya Zanzibar ina Wajumbe wawili katika Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ambao muda wao wa kutumikia bodi hiyo haujamalizika. Wizara haina ofisa anayeshughulikia mikopo ya elimu ya juu katika Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na haina taarifa ya kustaafu kwake. Hata hivyo, katika Idara ya Elimu ya Juu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Wizara ilikuwa na ofisa anayeshughulikia elimu ya juu ambaye hivi sasa amestaafu kwa kukamilisha utumishi wake. Ofisa huyo aliwahi kuomba kuongezewa muda wa utumishi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano bila ya mafanikio. Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu kama ifuatavyo:-

a) Kama nilivyotangulia kusema ofisi ambayo ofisa wake alikuwa anafanya kazi haihusiani na mikopo ya elimu ya juu. Hata hivyo, hakukuwa na athari yoyote kwa wanafunzi wa Zanzibar kupata mikopo ya kwenda kusoma vyuo vya nje ya Tanzania.

b) Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, haitoi mikopo kwa wanafunzi kusoma nje ya Tanzania isipokuwa katika baadhi ya nchi ambazo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetiliana Mkataba Maalum na nchi hizo kama vile Urusi, China na Uturuki. Nafasi hizo zinapotangazwa kila mwanafunzi mwenye sifa anayo haki ya kuomba. Wanafunzi wa Zanzíbar waliopitia Jamhuri ya Muungano wanaosoma Urusi na Ukraine ni wanafunzi 28.

c) Wizara tayari imeshawasilisha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi jina la ofisa mwengine atakayekamata nafasi ya ofisa aliyestaafu katika Idara ya Elimu ya Juu na wala sio Bodi ya Mikopo.

Nam. 110

Ukosefu wa Mashine za *ICU* Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza**:-**

Chumba cha wagonjwa mahututi katika Hospitali ya Rufaa Mnazi Mmoja kwa zaidi ya miaka minne hakina mashine maalum za kusaidia wagonjwa mahututi baada ya iliyokuwepo kuharibika. Serikali iliahidi kurejesha huduma hiyo haraka.

(a) Je, ni kitu gani hasa kimesababisha mashine hizo kutotengenezwa hadi sasa wakati tukisubiri Mradi wa Ujenzi wa *ICU* kutoka Jamhuri ya Watu wa China.

(b) Kuna taarifa kuwa kampuni mbili zilijitokeza na kueleza kuwa zina uwezo wa kuzifanyia matengenezo mashine zilizoharibika, kutoka Mkoani Arusha na Dar-es-Salaam. Je, hatua gani zilizofikiwa hadi sasa baada ya kampuni hizo kujitokeza.

(c) Wizara ya Afya kwa kuzingatia umuhimu wa mashine hizo ina mpango gani wa dharura wa kuondoa tatizo hilo mbali na mpango wa muda mrefu wa kusubiri msaada wa Serikali ya China.

(d) Kwa kuwa tatizo hilo ni la muda mrefu na Serikali inasema iko mbioni bila ya mbio kumalizika. Kwa nini Wizara ya Afya isiitishe harambee ya wananchi, wahisani na wafanyabiashara kuchangia gharama za mahitaji ya *ICU* Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Afya - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 110 lenye vifungu (a), (b), (c) na (d) kama hivi ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, mashine za *ICU* zilizokuwepo ambazo hivi sasa tunazikongoa tunatia mpya zina umri wa miaka 15 tangu zifungwe, kwa hiyo umri wake wa kufanya kazi umekwisha na kwa sasa zote haziwezi kufanya kazi. Pia mafundi wetu walikuwa na uwezo mdogo wa kuzitengeneza mashine hizo zilipokuwa zinaleta matatizo.

b) Ni kweli kampuni mbili ziliwahi kueleza kuwa zina uwezo wa kutengeneza lakini wakati ilipotolewa tenda ya kufanya upembuzi yakinifu wa kuweka *oxygen ICU, theatre, emergency room* na *maternity* kampuni hizo zilitolewa hatua za awali wakati wa kutathmini tenda hizo kwa kutowasilisha vigezo vinavyostahiki kama tenda ilivyoagiza. Hivyo, kwa kuwa mashine hizo zimechoka Wizara iliona kuna haja ya kupatikana mashine mpya za kisasa ambazo zitakuwa na uhakika kuliko kutumia fedha nyingi kwa matengenezo ya mashine chakavu. Kwa kuhakikisha wataalamu wetu wanapata ujuzi, baadhi yao walikwenda nchi za nje Norway wakapata mafunzo angalau ya *maintenance* ya kuja kuzitengeneza mashine zitakazofungwa.

c) Wizara imeshatiliana mkataba na kampuni mbili kutoka Dar-es-Salaam, moja kuleta vifaa na nyengine kuweka mtandao wa *oxygen*. Malipo ya awali yameshafanyika, vifaa vinafungwa, namuomba Mhe. Mwakilishi tukitoka hapa tufuatane aende akakague.

d) Wizara inafanya shughuli zake kiserikali na wanaosaidia hufuata taratibu za kiserikali kutoa misaada, lakini kwa kuwa tatizo hili ni gumzo la kudumu nawaomba wanaoguswa hasa Mhe. Jaku Hashim Ayoub tushirikiane na tutashukuru wahisani na wafanyabiashara kama watafanya harambee na kuipa Wizara kama wanavyoleta wengine bila ya kuombwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa mashine zilikuwa na muda wake maalum wa matumizi kama alivyojibu Mhe. Waziri katika swali la msingi.

(a) Je, Mhe. Waziri, huoni kwamba serikali haikuchukua hatua hizo mapema kununua mashine hizo ili kuweka spea, hata gari yako nafikiri ina mpira mmoja spea nyuma.

(b) Kwa kuwa mashine hizo zina umuhimu mkubwa katika kusaidia wagonjwa na tumekuwa tukishuhudia wagonjwa wengi wanaoingia mle hupoteza maisha. Je, Mhe. Waziri huoni kwamba hilo tatizo ni la muda mrefu.

(c) Ulitoa kauli kama sitokosea baada ya miezi sita kama haitofika utajiuzulu kutengenezwa *ICU*. Je, Mhe. Waziri, kauli hiyo iko vile vile.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, lile la kwanza sikulisikia vizuri lakini nakumbuka kama alisema kufuata spea kwa wale waliozileta kama ndivyo nilivyomfahamu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kwa kuwa mashine hizi zilikuwa na muda wake maalum wa matumizi kama alivyojibu Mhe. Waziri katika swali la msingi. Je, kwa nini serikali haikuchukua hatua mapema kununua mashine mpya kabla muda wa matumizi kumalizika.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kununua spea wakati huo mimi nilikuwa sipo kwa hivyo waliokuwepo kama ilikuwa ni kununua spea ilikuwa zinunuliwe wakati huo. Ninachojua kwamba muda wake ni mrefu miaka 15 na zilipokuja zilikuja kama msaada kutoka kampuni moja ya Marekani wakati huko tayari zilikuwa ni *recondition*. Sasa kutengeneza kitu kibovu pengine hata hizo spea kwenye viwanda hakuna na ndio maana uamuzi ukaja aidha moja Wachina watujengee mpya au zile pale tununue mashine nyengine na mashine hizo nyengine zimo katika kufungwa.

Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi alisema kwamba ni muda mrefu tangu kutolewa ahadi hii. Mhe. Spika, shughuli hiyo inaendelea na kama nilivyosema mashine hizo zinafungwa hivi sasa.

Mhe. Spika, swali la tatu naomba Mhe. Mwakilishi arudie kwenye *hansard* sikusema nitajiuzulu baada ya miezi sita, nilisema kama bajeti ya 2011/2012 itamalizika hakuna *ICU*, bajeti nyengine haijafika na ikifika ninahakika kila kitu kitakuwa tayari kama nilivyoahidi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, kwanza naishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar kuona suala hili la *ICU* kama lina muda mrefu na sasa hivi linashughulikiwa. Naipongeza na inshaallah Mwenyezi Mungu atatujaalia tupate mafanikio.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali amesema kwamba mashine zilizokuwepo za zamani zilikuwa zina uhaba wa mafundi matengenezo ilikuwa yanawapa tabu. Sasa kwa sababu tunafungiwa mashine nyengine mpya. Je, Mhe. Waziri, tayari ameshapeleka wataalam wa kujifundisha ili pindipo ikiharibika waweze kutengeneza. Kama hawajapelekwa ni lini watapelekwa wataalam wa kujifundisha ili mashine itakapoharibika tuwe tuna mafundi wa kudumu wa kutengeneza.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, katika jibu mama nilieleza kwamba tulishawapeleka wafanyakazi wetu Norway kujifunza. Kwa kawaida hawa wanaotufungia mashine nyengine hivi sasa na wao watatakiwa kabla zile mashine hazijaanza kazi wawafundishe mafundi wetu na kuwaeleza jinsi ya kutengeneza matengenezo madogo madogo. Bahati nzuri kampuni inayofunga hizi mashine za sasa ipo Dar-es-Salaam na itakuwa rahisi kuweza kuwaita wakati wowote linapotokea tatizo tofauti na wale walioko Marekani Georgia.

Nam. 161

Mjamzito Kujifungua nje ya Wodi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza**:-**

Gazeti la Serikali la Zanzibar Leo tarehe 23/2/2012 ukurasa wa kwanza imeripotiwa mama mjamzito kujifungua nje ya Wodi ya Wazazi baada ya wauguzi na madaktari wasaidizi kukataa kumpokea kutokana na kwenda hospitali akiwa hana vifaa vinavyotumika kwa mama wajawazito kabla ya kujifungua.

(a) Je, Mhe. Waziri, nini ukweli wa kuhusiana na suala hilo na hatua gani zimechukuliwa kwa watu waliofanya ukatili huo.

(b) Kwa kuwa Wajumbe wa Baraza wamekuwa wakilalamikia suala la wazazi kutozwa ada kwa muda mrefu. Je, Mhe. Waziri, huoni tukio hilo linahalalisha malalamiko hayo na kwamba sasa ipo haja ya kutoa huduma zote kwa wazazi bila ya malipo.

(c) Kwa kuwa kesi za uzazi ni kupona au kifo. Je, baada ya tukio hilo kutokea hatua gani Wizara imechukua ya kumfariji na kumpa mkono wa pole kutokana na vitendo alivyofanyiwa na wafanyakazi wa Wizara ya Afya.

Mhe: Waziri wa Afya – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 161 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Ni kweli tukio limetokea, limeripotiwa kwenye vyombo vya habari na aliyefanyiwa aliandika barua kwa uongozi wa Hospitali na Wizara kulalamika.

Hatua zilizochukuliwa:-

- Kamati ya nidhamu iliitishwa tarehe 27/2/2012 na Wajumbe wawili Mkuu wa Wodi na msaidizi wake walialikwa na barua ya mlalamikaji ilisomwa.
- Mlalamikaji na mzazi muhusika walijieleza.
- Walalamikiwa walisomewa barua ya malalamiko dhidi yao nao wakajitetea.
- Mwishowe wakaitwa wote kwa pamoja walalamikaji na walalamikiwa na wote wakajieleza na walalamikiwa hawakukubaliana na hoja za walalamikaji kwamba wamewafukuza na kuwatukana. Kamati ya nidhamu iligundua mambo yafuatayo

- Wafanyakazi wamefanya makosa ya kinidhamu na hawakuleta mkabala mzuri mbele ya mzazi na wakatiwa hatiani kwa makosa ya kukiuka maadili yao ya kazi kwa mujibu wa sheria za utumishi kwa umma nambari 2 ya mwaka 2011, sura ya 7 kifungu nambari 82(1)(a) nambari 35 ya ukiukwaji wa maadili na nidhamu.

- Iliamuliwa wapewe onyo kwa maandishi na waondolewe katika kituo cha kazi mara moja.

(b) Uhalali wa malalamiko hayo hautokuwepo mara tu kutakapotoka maelekezo mengine kuhusu sera ya uchangiaji na nani achangie na nani asichangie.

Mhe. Spika, kwa taarifa ya wajumbe niliahidi kwamba nitamaliza muongozo juu ya uchangiaji huu hapa bado naufikisha serikalini, nadhani itakapofika bajeti itakuwa suala hili limemalizika.

(c) Mzazi pamoja na aliyemleta waliombwa radhi kwa usumbufu walioupata na kuhakikishiwa kwamba wizara itachukua hatua za kinidhamu kwa makosa waliyofanya wafanyakazi wake, ili iwe fundisho kwa wengine.

Kwa ufupi hatua zimechukuliwa kama utaratibu wa serikali mambo ya kiutumishi yanavyostahiki kufanyika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuwa suala la mama wajawazito kuchangisha huduma za uzazi limekuwa likipingwa na wajumbe wa Baraza hili kwa muda mrefu.

(a) Kwa nini serikali imepata kigugumizi kutokufuta uchangishaji huo na sheria ipi iliyopitishwa katika Baraza hili la Wawakilishi wajawazito hao kuchangishwa.
(b) Je Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kwamba kuna kikao nilikuambia kuwa kuna wananchi huweka rehani vitu vyao ili kupata huduma za uzazi, kwa maana hiyo utakubaliana na mimi kuwa hiki kitu kipo hivi sasa.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, serikali inapata kigugumizi. Mhe. Spika, hebu arejee swali lake hili.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe rejea swali kidogo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kwa kuwa suala la mama wajawazito la kuchangisha huduma za uzazi limekuwa likipingiwa kelele na wajumbe wa Baraza hili kwa muda mrefu.

Kwa nini serikali imepata kigugumizi kutokufuta uchangishaji huo na sheria ipi iliyopitishwa na Baraza hili kuchangishwa huduma hiyo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, serikali haijapata kigugumizi. Serikali inatekeleza maagizo ya Baraza hili, na Baraza hili ndilo lililopitisha uwamuzi kwamba wananchi wachangie, katika kikao cha mwaka 2001, mwezi siukumbuki vizuri, lakini iliamuliwa katika hili tulipokuwa tukipitisha sera ya afya, kwamba wananchi wachangie. Kwa hivyo, halikufanywa kibabe, lilifanywa kwa uamuziwa Baraza hili.

Kwa hivyo, hatuna kigugumizi, kilichokuwa kinatakiwa ni mfumo utakaokuwa na uhakika yule anayechangishwa, anachangishwa vipi, kiasi gani na kwa sababu gani. Mhe. Spika, naomba kidogo unipe nafasi ili niweze kumjibu Mhe. Jaku ameuliza maswali maswali yake vizuri.

Tumefanya uchunguzi wa kiasi gani fedha zinazotakiwa kwa kuhudumia sehemu ya wazazi tu peke yake na gharama ziwe vipi. Kwa mwaka tunahitaji sio chini ya shilingi milioni 850, kama kila kitu kinatakiwa kiwe murwa. Lakini sio kwa hospitali nzima ya Mnazi Mmoja kwa kitengo cha uzazi tu ambacho kipo hospitali ya Mnazi Mmoja na Mwembeladu, tunahitaji sio chini ya milioni 850.

Sasa Mhe. Spika, ninachotaka kukifikisha serikalini ni kwamba aidha pesa hizi zote ziwe sehemu au zilipwe maalum kwa kitengo hicho, ambapo hali ya bajeti naamini haitowezekana na kwa kiasi gani basi wananchi walipie. Je, walipie asilimia 10 ya gharam au asilimia 20 ya gharama au asilimia 30 ya gharama au asilimia 50 ya gharama. Hilo litakuwa ni agizo la serikali hatuwezi kulifanya wizara peke yetu. Lakini nimeshamaliza pamoja na wataalamu wangu kila kitu kuhusu muongozo na jinsi ya kuchangia.

Lakini tusisahau Mhe. Spika, kwamba wananchi wengi kama vile anavyosema, wananchi wengi hawana uwezo wa kulipia gharama kamili. Kutakuwa na kundi kubwa litakalobidi lisamehewe. Swali, hakuna *free lunch*, kama anasamehewa mmoja basi mwengine ni lazima alipe. Je, italipa serikali au Mhe. Jaku na Juma Duni. Kwa wastani kwa mwezi tunahitaji si chini ya milioni 70, kama ni ushauri utakaokubalika basi tukubaliane Wazanzibari wote kila mmoja achangie angalau shilingi 10, ili pesa zile ziende kwenye mfuko maalum kwa *maternity* ili gharama hizi ziondoke. Lakini vinginevyo aidha itakuwa ni serikali au mwananchi mwenyewe anayekuja kujifungua, itabidi kwa kiasi fulani agharimie.

Mimi mwenyewe Mhe. Spika, napenda iwe bure, jumuiya za kimataifa zinapenda uzazi uwe bure, lakini ni suala la uwezo. Kwa hivyo, naomba niachiwe nimalizie shughuli hii ikamilike, nitaeleza hapo Mwenyezi Mungu akitujaalia pengine wakati wa bajeti na nitakuwa nimeshapata muongozo wa serikali jinsi ya kulipia gharama hizi. Lakini hakuna kigugumizi, na sera ya kuchangia imepitishwa na Baraza hili, kwamba wananchi wachangie huduma za afya.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Swali langu nambari 2 halijapata jawabu Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Afya: Swali lipi hilo.

Mhe. Spika: Hebu rudia swali Mhe. Mjumbe.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Je, utakubaliana na mimi Mhe. Waziri kwamba hapo mwanzo watu walikuwa wakiweka rehani vitu vyao, ikiwemo simu na vyombo vyao vya dhahabu ili kupata huduma hii ya uzazi. Nilikuwa nataka kupata jawabu hilo. Ni kweli au sio kweli.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, sikubaliani na Mhe. Mjumbe kwamba watu walikuwa wakiweka rehani.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ili niweze kumuuliza Mhe. Waziri wa Afya swali moja la nyongeza. Kwanza kabla ya kumuuliza swali hilo, naomba nitumie nafasi hii ili kuipongeza Wizara ya Afya kwa hatua walioichukua juu ya mzazi huyo ambaye alipata matatizo wakati alipotaka kujifungua.

(a) Mhe. Spika, swali langu liko hapa. Je, Mhe. Waziri hali ya mzazi huyo ambaye amejifungua mpaka sasa ikoje na kile kizazi alichokizaa mpaka muda huu hali yake ikoje.

(b) Kwa kuwa suala la kinamama kujifungua ni suala la kitaifa, ambalo linamgusa ama mwanamke au mwanamme na kwa kuwa Mhe. Waziri umesema kwamba bajeti ya milioni 800 ni kubwa haiwezi kulipika.

Je, serikali haioni kwamba iweke kipaumbele kwa fedha hizi katika bajeti yake, ili suala hili la kinamama wajawazito likaondoa matatizo haya na zaidi ukizingatia kwamba wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi wamekuwa wakililalamikia sana jambo hili.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, taarifa tuliyonazo ni kwamba yule mama yuko salama na mtoto yuko salama.

Mhe. Spika, kuhusu suala la kipaumbele ni kuwa tatizo tulilonalo ni kwamba vipaumbele ni vingi, lakini katika vipaumbele vingi, vipaumbele vya kuzaa taifa la kesho ni kipaumbele cha kwanza, ni suala la maamuzi. Sisi tutajitahidi tutakapofikisha bajeti yetu wizara ya fedha kulieleza hilo na kama nilivyoeleza, hivi sasa nimo mbioni kuweka waraka kuwaeleza serikali.

Kwa hivyo, itategemea uwezo wa serikali lipi liwe mwanzo na lipi liwe la pili. Maana moja katika tatizo ambalo Waheshimiwa Wajumbe huwa wanatuhimiza ni wagonjwa kupelekwa nchi za nje, ambao na wao vile vile ni maisha ya wale waliohai. Kwa hivyo, itategemea kipi kiwe cha kwanza na kipi kiwe nambari mbili inategemea na uwezo wa serikali.

Lakini Mhe. Spika, naomba kuwathibitishia Waheshimiwa Wajumbe, kwamba liko juu ya meza yangu nalifikisha serikalini, litajadiliwa na nina uhakika wakati wa bajeti tutalieleza na tutalichambua kwa vizuri zaidi nini tufanye ili suala hili lipate ufumbuzi wa kudumu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba kulitokea uzembe katika kumuhudumia mzazi huyu na kwa kuwa ulimwengu mzima una-*advocate* hali ya afya ya mama na mtoto.

Je, Mhe. Waziri anaweza kutueleza kuwa hii hatua ya kumuondosha huyu aliyehusika na uzembe huu ni wamemuondosha hospitali ya Mnazi Mmoja na wamempeleka kituo gani. Hilo la kwanza.

La pili, je kama kifo cha mmoja kati ya hao wawili, aidha mama au mtoto kingetokea. Je, hukumu ya kumuondosha Mnazi Mmoja na kumpeleka Makunduchi au Kivunge ingetosha kukidhia roho ya mmoja kati ya hao.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nasikitika hili swali la kwanza sikulisikia ni kupelekwa mahakamani.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, swali langu la mwanzo lilikuwa ni kwamba huyo aliyehusika na uzembe huu je, amehamishwa kutoka hospitali ya Mnazi Mmoja na kupelekwa wapi, hilo ndio lilikuwa swali langu. Maana adhabu aliyopewa kwa mujibu alivyojibu Mhe. Waziri, ni kwamba wamemuhamisha katika kituo cha kazi, lakini hakutaja wapi walipompeleka.

Sasa je, huyu mzembe aliyekuwa anataka kuhatarisha maisha ya mama na mtoto, ameondoshwa hospitali ya Mnazi Mmoja na kupelekwa wapi. Moja lilikuwa ni hilo.

La pili, kwa sababu uzembe kama huu ungepaswa kukomeshwa pale ulipoanza. Je, yeye anahisi Mhe. Waziri kwamba kumuhamisha mzembe anayetaka kutoa maisha ya mzazi au mtoto, aidha kumtoa hospitali ya Mnazi Mmoja na kumpeleka hospitali ya Makunduchi, au kumtoa hospitali ya Mnazi Mmoja na kumpeleka hospitali ya Kivunge, je ingetosha kufidia roho ya mmoja kati ya hao. Hilo lilikuwa ni la pili.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, wafanyakazi hawa kwa taarifa ni moja katika wafanyakazi hodari sana katika kitengo cha uzazi na kwa kweli walisikitika na kujutia kwa lile lililotokea. Mimi ningeshauri kwamba nifuatane na baadhi ya Waheshimiwa Wawakilishi, ili twende pale kwenye kitengo cha uzazi usiku na tuone jinsi inavyowaelemea wale wafanyakazi kazi hizo.

Mhe. Spika, kuna upungufu mkubwa wa wafanyakazi katika sehemu ya uzazi na wanahitajika waengezwe. Kwa hivyo, kutokana na presha ya kazi inayotokea pale, wale vijana walisikitika na kujutia yale yaliyotokea. Ni moja katika wafanyakazi hodari wanaofanya kitengo kile. Kwa hivyo, hatukuwapeleka Makunduchi wala kwengine.

Hospitali ya Mnazi Mmoja ina vitengo visivyopungua 18 na kuna upungufu mkubwa wa wauguzi, hivyo tumewabadilisha eneo tu.

Mhe. Spika, kuhusu suala la kwamba wangefariki au kutofariki Mwenyezi Mungu ameliepusha na hatuwezi kupima uwezo au thamani ya mwanadamu kwa kumtia adabu mfanyakazi. Lakini hata hivyo naomba tuelewe kwamba tumepitisha sheria ya utumishi hapa hapa na kuna taratibu za kikazi na kisheria kufuatwa, hatuwezi kukurupuka suala la mwanzo ukasema mfukuze au mfanyenini. Kuna taratibu za kisheria zilizowekwa na hizo nimetaja mpaka vifungu ambavyo tumefuata. Jana na juzi tumekuwa tunajitahidi sheria zifuatwe, isiwe sheria zifuatwe kwa mmoja tu, lakini iwe kwa pande zote.

Nam. 104

Huduma ya Maji Safi na Salama

Mhe. Asha Bakar Makame – Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla ya yote nichukuwe nafasi hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kuamka katika hali ya afya njema. Baada ya hayo Mhe.Spika, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii. Naomba Mhe. Spika, kwa idhini yako nijibiwe swali langu nambari 104.

Kwa muda mrefu wananchi wa Mazizini, Kiembesamaki, Mbweni na Chukwani wamekosa huduma ya maji safi na salama. Katika awamu iliyopita Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ilichukua jitihada ya kuwapatia huduma hiyo muhimu, lakini baada ya muda mfupi huduma hiyo ilisita na hadi sasa wakaazi wa maeneo hayo wanaendelea kutaabika na utafutaji wa maji.

(a) Ni zipi sababu za kukatika kwa huduma hiyo muhimu kwa jamii.
(b) Mhe. Waziri unalieleza nini Baraza hili tukufu pamoja na wananchi wa shehia hizi kuhudu utatuzi wa suala hilo.
(c) Je, huoni kwamba kuwakosesha wananchi maji safi na salama ni kuwanyima fursa yao ya kufaidi matunda yao ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati –Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 104 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, wananchi wa Mazizini, Kiembesamaki, Mbweni, Chukwani wanapata huduma ya maji safi na salama kutoka katika visima vya Kiembesamaki. Mhe. Spika, kushuka kwa uzalishaji kunatokana na tatizo liliopo la umeme, linalosababisha kuungua kwa moja ya pampu inayosukuma maji katika kisima hicho.

(b) Mhe. Spika, napenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi pamoja na wananchi wengine wa shehia hiyo, kuwa wizara yangu inaendelea na juhudi za kulitatua tatizo hilo, ili kuwaondoshea shida inayowakabili.

(c) Mhe. Spika, wizara yangu lengo lake hasa ni kutekeleza kwa vitendo ilani ya uchaguzi ya CCM na kuhakikisha inafikia malengo ya millenium, sambamba na hilo inahakikisha kwamba wananchi wote wa Unguja na Pemba, Mijini na Vijijini wanafaidika na matunda ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964.

Mhe. Asha Bakar Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nichukuwe nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri, kwa sababu suala hili kwa kuwa ni mimi nilikuwa ni miongoni mwa waliokuwa hawapati maji. Lakini nashukuru wamechukua jitihada na kwamba sasa maji napata.

Lakini je, ni sababu zipi za msingi ambazo zinaleta katika sehemu hizi baadhi ukitoka kwenye nyumba moja wengine wanapata maji na nyumba ya pili hawapati maji. Ni sababu zipi hasa za msingi zinazosababisha kufanya hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika. Mhe. Spika, sababu inayopelekea kupungua kwa maji katika eneo hilo ni kuungua kwa pampu katika kisima cha matrekta.

Wizara yangu kupitia mamlaka ya maji, tayari imeshaagizia pampu hiyo na wakati wowote itafika Zanzibar. Mhe. Spika, itakapofika tu pampu hiyo tutaelekea huko kwa kuifunga na tunaamini kwamba maji yatatoka kama ambavyo yalikuwa yanatoka katika kipindi cha awali.

Kwa hivyo, Mhe. Mjumbe naomba vuta subra na waelimishe wananchi wako kwamba wavute subra na wao.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa ya kuweza kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Spika, zamani idara ya maji ilikuwa inafanya utaratibu wa kuhifadhi maji yake katika matangi. Yanapotoka katika vianzio vyake yale maji yanahifadhiwa kwenye matangi., halafu ndio yanashushwa kwa wananchi.

Sasa wizara kwa sasa ina mpango gani wa kuweza kurejesha huduma ile ili kuweza kuipunguzia kazi kubwa ambayo mashine zile zinafanya kazi kwa muda wa masaa yote na watu wakawa hawatoshelezeki na maji. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, wizara yangu kupitia mamlaka ya maji, katika juhudi nilizozifanya ni kuongeza visima na kuongeza matangi. Kwa hivyo, baada ya kuongeza hayo matangi, basi tayari tuna ukusanyo mkubwa zaidi kukusanya maji na kuwapelekea wananchi, tofauti na kile kipindi cha nyuma ambapo tulikuwa tunatumia matangi mawili tu yaliyokuwepo Saateni. Sasa hivi tuna matangi mengi zaidi, na tunapata mkusanyo mkubwa na tuna fursa nzuri ya kuwagawia wananchi kwa vile inavyostahiki.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini niongezee majibu ya nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, licha ya jitihada mbali mbali zinazochukuliwa na wizara hii katika kuhakikisha kupatikana kwa maji kwa wananchi vizuri zaidi. Serikali pia ina mpango wa kubadilisha paipu zile za zamani ambazo ndio chanzo kikubwa cha kupungua maji kuweza kusambaa vizuri kwenda katika maeneo mbali mbali, kutokana na kujaa kwa *calcium.* Hivi sasa serikali inachukua hatua ya kubadilisha miundombinu hiyo, ili kuweka miundombinu ya kisasa kwa ajili ya kuwapatia wananchi maji safi na salama na kwa vizuri zaidi.

Nam. 162

Matengenezo ya Nyumba Mji Mkongwe

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Serikali na wananchi wamekuwa wakichukua hatua mbali mbali za kuyafanyia matengenezo majumba yanayokabiliwa na uchakavu katika Mji Mkongwe wa Zanzibar, lakini kumeibuka tatizo la kuzungushwa mabati bila ujenzi kufanyika katika muda muafaka katika baadhi ya majengo

Je, serikali imechukua hatua gani kwa mabati yaliyozungushwa katika jengo moja la Forodhani, jirani na jengo la zamani la Shirika la Umeme, ambalo limezungushwa mabati muda mrefu na kuibana barabara ya Malindi Forodhani na kuleta usumbufu kwa watumiaji wa barabara hiyo kwa kuweka foleni ya magari.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Spika, idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 162 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe, imekuwa ikitoa ruhusa ya kuzungusha mabati, kwa majengo yanayofanyiwa ukarabati mkubwa katika eneo la Mji Mkongwe kwa ajili ya usalama wa majrani pamoja na wapiti njia. Jengo liliopo jirani na jengo la zamani la Shirika la Umeme Forodhani, kwa muda mrefu limekuwa katika ukarabati mkubwa kutokana na jengo hilo kuwa katika hali mbaya sana, hata kufikia kuporomoka kwa upande mmoja wa mbele wa jengo hilo. Lakini hivi sasa liko katika hatua za mwisho na wakati wowote kuanzia sasa mabati hayo yataondolewa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya kutokuridhisha ya rafiki yangu Mhe. Naibu Waziri. Nafikiri jengo lenyewe atakuwa hajalifahamu.

Mhe. Spika, hilo jengo lipo karibu miaka minne limezungushiwa mabati, hata kama ni nyumba ya ndege inayochukua kijiti kimoja kimoja basi ingekuwa imeshamalizika. Mhe. Spika, barabara ile tumekuwa tukiipigia kelele kwa muda mrefu sana na Mhe. Dk. Mwinyihaji ni shahidi wa suala hili, kila siku anachezea maswali kuhusu barabara ile.

Hilo jengo Mhe. Naibu Waziri nafikiri hujalifahamu. Sijui utakuwa tayari baada ya kikao hiki nikakuoneshe jengo hilo. Ofisi ya Utumishi ya Chuo kilichokuwepo, nyumba ya kwanza nyumba ya pili ndio jengo lenyewe hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika. Kwanza niongezee kumjibu Mhe. Mjumbe kwamba katika swali tumefahamu kuwa jengo lililo karibu na Shirika la Umeme la zamani, kwa hviyo tumefahamu kama hivi ambavyo tumejibu. Lakini kama itakuwa silo tulilojibu basi naomba nishirikiane na Mhe. Mwakilishi tuondoke kwa pamoja na akanioneshe sehemu hiyo, ili tupate kulifanyia kazi.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi nimuulize swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa jengo alilokuwa akilizungumzia Mhe. Jaku linafanana na lile ambalo liko pale Mambo Msiige pale ambalo limezungushwa mabati.

Je, uko tayari na jengo lile yale mabati kuondoshwa.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, twende kwenye jengo ambalo swali hili linahusika. Ahsante tunaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura, kunipa nafasi hii nikazungumza nikiwa mjumbe wa mwanzo kuchangia ripoti hii ya kamati kwa asubuhi hii.

Mhe. Spika, mimi nataka niseme kwamba kuna jambo ambalo sisi kama wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, pamoja na serikali kujifunza hasa kwa tukio hili ambalo lilisababisha kuundwa hii kamati.

Mhe. Spika, nadhani moja katika chanzo ambacho kilichochangia kuundwa kwa kamati hii ni ukiukwaji wa kanuni zetu za Baraza. Mhe. Spika, mara nyingi tunapokuwa tunauliza maswali mbali mbali Barazani, basi maswali haya huwa tunauliza kwa niaba ya wananchi, kwa sababu wananchi wengi wao ambao wanaotusaidia kuuliza haya maswali ni watendaji au wafanyakazi wa serikalini. *(Makofi)*

Kwa hivyo, haya maswali tunayouliza Mhe. Spika sio kama ni maswali ya kwetu, isipokuwa ni maswali ya wananchi na wakati mwengine wanakuwa wameshachoshwa na yale mambo yanavyofanyika. Vile vile wanashangaa kwamba sisi Wawakilishi wao tupo, lakini tunashindwa kuyasemea na bado yanaendelea.

Mhe. Spika, nadhani sisi kama Kamati au Wajumbe wa kamati uliotuteua tulikuwa kama walivyosema wenzangu kwamba sisi tulikuwa kama ni madaktari, ambao tuliletewa mgonjwa na tukaambiwa tumpime, tuangalia maradhi yake, sasa tumetayarisha na cheti ambacho tunakipeleka dirishani kwa ajili ya dawa.

Kwa hivyo, cheti chetu ni hili *document* ambalo tulilokuletea Mhe. Spika pamoja na vile vielelezo ambavyo hata na wewe mwenyewe ilibidi utafute msaidizi wa kuweza kukusaidia kubeba vile vielelezo. Kwa kweli hii tuliifanya kwa makusudi kwa ajili ya kuondosha utata na kupunguza maswali mengi ambayo yasiyokuwa na jawabu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kutokana na ugumu wa kazi hii uliyotupa, kwa kweli tulipata wakati mgumu sana kuifanyakazi hii na hasa ukiangalia mfumo wetu wa utawala kwamba serikali inatoka ndani ya Baraza la Wawakilishi, yaani nakusudia mawaziri tofauti na ile mifumo ya wenzetu, kwamba Rais anateua mawaziri ambao wanakuwa sio Wabunge au Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Kwa hivyo, utakuta tunajichunguza sisi wenyewe kwa wenyewe, ndio maana nikasema tulipata wakati mgumu katika kulifuatilia suala hili. Kwa maana hiyo, tulijaribu kutafuta kila *evidence* ambayo itakayoweza kutuondoa katika lawama yoyote itakayotokezea wakati wa kazi yetu.

Mhe. Spika, tulithubutu kununua *tape recorder*, ili iwe shahidi wetu namba 2, kwa sababu masuala haya mtu anaweza kusema na baadaye kuyakanusha na sisi tulikuwa wazi kabisa kwamba mtu tunamwambia, tunazungumza tunaandika, lakini na hii *recorder* inakusikia maneno yote ambayo unayoyasema. *(Makofi)*

Kwa hivyo, hii inakuwa kama ni shahidi hata ikitakuwa ushahidi Mahakamani, basi na *tape recorder* hii tutaipeleka. Hivyo, hii tuliifanya kwa makusudi, ili kuonesha kwamba tulikuwa hatuna utashi katika kutekeleza kazi yetu.

Mhe. Spika, mimi nikiwa Mjumbe wa Kamati naiambia serikali kwamba mgonjwa wetu, yaani serikali yetu tumeangalia matatizo yake kama wengine walivyosema kwamba hii tumekwenda kwa wizara zaidi mbili tu, lakini hii *diagnosis* kwa serikali nzima. *(Makofi)*

Sasa sisi tunapeleka cheti kwa daktari na daktari wetu ni Makamu wa Pili wa Rais. Kwa hivyo, inategemea dirishani kama dawa, basi maradhi yatapoa, lakini kama hakuna dawa maradhi yataendelea. Mhe. Spika, sisi tunaikabidhi hii ripoti serikali kwa ajili ya kuifanyiakazi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakuja katika hoja kwa sababu nataka nimpunguzie kazi kidogo Mhe. Mwenyekiti wangu kwa kutoa ufafanuzi nitaanza na kwa swahibu yangu ambaye ni rafiki yangu Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Kwa kweli namshukuru ametupongeza Kamati, lakini pia ametutahadharisha na huo ndio wajibu wetu, kwa sababu unapokwenda safari usitegemee kuwa safari ile utafika salama, kwani njiani vimo vikwazo mbali mbali, sasa unapopata ushauri wa wenzako inabidi ushauri ule uuchukue na uufanyie kazi, tunakushukuru sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Vile vile alitoa ushauri katika ile sehemu tuliyozungumzia zaidi wale vijana ambao si waajiriwa wa serikali, lakini ile Kampuni ya Ubebaji wa Mizigo. Mhe. Spika, hapa kidogo nataka nitoe ufafanuzi, ili wenzetu wajue kwa nini tulifanya *conclusion* ile ya kwamba angalau serikali iwawezesha wale vijana kununua asilimia 50, Mhe. Mjumbe alisema ah! Masuala hayo itakuwa kama tunafanya upendeleo kwa kikundi fulani, kwa sababu wako Wajasiriamali wengi je, serikali wote itawawezesha.

Lakini sababu gani iliyotufanya kwa nini tukasema serikali itumie utaratibu wa kuwawezesha. Tumefanya hivi kwa sababu serikali yenyewe imeunda Wizara maalum kwa ajili ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. *(Makofi)*

Vile vile kwa wale vijana ambao tumeiomba serikali iwasaidie na kuwasaidia inaweza ikawapa aidha *guarantee* au hata kwa *cash*, yaani kuweza kumiliki asilimia 50 ya *share* ya ile kampuni iliopo.

Mhe. Spika, vijana hawa ndio waanzilishi wa Kampuni ya Kubeba Mizigo pale Uwanja wa Ndege na kwanza walikuwa wakifanyakazi kienyeji na baadaye wakapata ushauri, tena mwanzo walikuwa na mahusiano ya karibu sana na Mkurugenzi wa Uwanja wa Ndege. Mwisho Mkurugenzi aliwaambia hebu kaeni muunde ushirika, basi vijana wale wakaa na kuunda ushirika na kwenda kufanya usajili.

Kwa hivyo, walikuwa wakishauriana sana na Mkurugenzi aliyekuwepo wakati ule ndugu Malik. Mhe. Spika, baadaye wao wenyewe waliomba wapate msaada wa mzee mmoja ambaye yeye ni mtaalamu zaidi, yaani yeye ni mzoefu sana wa masuala ya mambo ya *Aviation*.

Sasa matokezeo yake walipomualika katika kile kikundi alikuja kama awe yeye ndiye mshauri wao, basi matokezeo yake yule akaja kuwageuka na kuunda yeye ile kampuni sasa badala ya wale vijana walioanzisha ule ushirika na hapo ndipo lilipokuja tatizo.

Mhe. Spika, hapo ndipo lilipokuja tatizo kwamba wale vijana ndio waliokuwa wakifanya ile kazi, lakini baadaye yule mwenzetu kutokana na maarifa pengine na uwezo wake, basi wao wakaja kuichukua ile kazi na wale vijana wakatakiwa waajiriwe wakati wao ndio waliokuwa ndio wenye ile kazi. Kwa hivyo, ina maana hapo ndipo likaingia sakata.

Vile vile ukiangalia katika ule mkataba katika zile *shares*, asilimia 10 ya *share holder* ya ile kampuni alikuwa ni mdogo wake Mkurugenzi wa Mamlaka ya Uwanja wa Ndege ndio yale tunayoyazungumza kwamba watu wanatumia ofisi kwa maslahi yao binafsi, wanaondoa vijana wale tena vijana wenyewe karibu 45 na walikuwa na familia zao. *(Makofi)*

Sasa leo unakuja kuwaondoa wale na kuchukua au unaanzisha kampuni nyengine na wale unawaweka nje wanakuwa kama ni wapagazi wako, kwa kweli hiyo tuiiona si halali.

Mhe. Spika, tuliona ah! Kwa nini tuendeleze *conflict* ambazo tayari zilikuwa zimeshaanza kupatiwa ufumbuzi na tuliona kwamba wale vijana wamewekwa nje na wao ndio waanzilishi wa ile kampuni, basi ndio maana tulishauri, kwa sababu wao wenyewe wale wanaomiliki ile kampuni walisema ah! Sisi tuko tayari kama wataweza kununua *shares* zetu zote basi hii kampuni wachukue wao, lakini wale vijana masikini ya Mungu hawana uwezo.

Kwa hiyo, ndio maana sisi tukasema kwamba hawa kusema tuachie wao itakuwa kama wamefutuka, hebu hivi sasa hii kazi wafanye wote kwa pamoja. Lakini wale wakadai kwamba sisi tayari tumenunua vifaa mbali mbali kwa ajili ya kubeba mizigo pamoja na vitu vyengine, hivyo watulipe *shares* zetu.

Sasa wale vijana ndio tukagundua kwamba wao wenyewe hawana uwezo, ndio maana tuliposema kwamba kupitia kwa bahati mbaya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika hayupo, lakini bado Mhe. Makamu wa Pili wa Rais yupo ambaye ndiye Kiongozi wa Shughuli za Serikali nadhani hilo ataliangalia kwa ukaribu, ili wale vijana wetu wasione kama.

Kwa kweli sisi serikali ndio tuliopitisha Sera ya Kuunda Vyama vya Ushirika, kwa sababu tunasema siku zote kwamba wananchi wajiunge na *SACCOS*, ili serikali iwawezeshe. Kwa maana hiyo, vijana wamejiunga na *SACCOS* na kuanzisha Mradi wao wa Kubeba Mizigo na wamekuja watu wenye uwezo wao na kuwapiga teke na kuwatoa nje.

Je, ile dhana au dhamira ya serikali kuanzisha hizi *SACCOS* au Vikundu vya Ushirika na halafu baadaye inapokuja neema tunawatoa nje, kweli ile dhamira ya serikali itakuwa imepatikana.

Kwa hivyo, hapa ndipo tulipochukulia kigezo kwamba serikali kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika wanayo mipango mingi. Kwa mfano, kuna Mikopo ya AK na JK na wale ni wananchi tena kwa bahati wanatoka maeneo tofauti ya Zanzibar.

Mhe. Spika, hiyo ndio iliyokuwa *concern* yetu na kupendekeza mapendekezo hayo.

Jambo jengine nataka Mhe. Mussa Ali Hassan ambaye ni swahibu wangu ameondoka leo kidogo. Kwa kweli jana yeye alijaribu kusema kwamba hii Kamati ilikuwa ichukue mambo mpaka ya Awamu ya Pili. Duu! tulisema Mhe. Mussa Ali Hassan hapa Baraza hizi Kanuni pamoja na Sheria zetu ameshazisoma.

Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi linaendeshwa kwa sheria na ndio maana kila baada ya miezi mitatu tunakuja hapa na tunakuja hapa Mhe. Spika bila ya majembe au mashoka ama sururu, isipokuwa tunakuja na midogo yetu, Katiba na Sheria ndizo zinazofanya sisi tulipwe mishahara.

Kwa hivyo, tunapokuja hapa Mhe. Spika, yapo mambo ya Awamu ya Kwanza tumeyarekebisha kwa mujibu wa sheria, Awamu ya Pili tumeyarekebisha kwa mujibu wa sheria, Awamu ya Tatu, Awamu ya Nne, Awamu ya Tano, Awamu ya Sita mpaka hivi sasa tuko Awamu ya Saba. Mhe. Spika, inaonesha Mhe. Mjumbe lile jambo aliloambiwa hakujua vya kulisema, kwa sababu alikuwa anakusudia kuwatetea watu, lakini unaposema twende katika mambo ya Awamu ya Pili.

Mhe. Spika, marehemu Mzee Abeid Amani Karume nilimsikia mwenyewe marehemu Mwadini nadhani alifariki na cheo cha *Captain*, alisema Mzee Karume alipita siku mmoja na kusikia sauti nzuri juu ya mnazi aloo ukiangua nyingi nitakupa mke wangu, basi sauti yake ilipokuwa nzuri, alimwambia wewe utakuwa Koplo wa Jeshi.

Mhe. Spika, kwa kipindi hicho ilikuwa right, lakini hivi sasa imba nyimbo zote atapiga Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein atakusikia utaimba kama atakwambia uende kwenye Jeshi basi kwanza lazima upite katika utaratibu ulioandaliwa, sasa mambo yanabadilika.

Kwa hivyo, sio kama mambo yaliyofanyika Awamu ya Pili ilikuwa sisi twende tukayafanyiekazi, kwa sababu sisi tulikuwa tukizungumza kwamba mambo mengi tuliyoyazungumza ni ukiukwaji wa Kanuni, Katiba pamoja na Sheria za nchi. Kutokana na hali hiyo, ndio maana tulizungumza sana ile Sheria ya *Procurement Act* ya mwaka 2005 imekiukwa. *(Makofi)*

Sasa kama kuna watu wamepewa mwaka 1964 na ndio maana katika Kamati kuna Wajumbe wengine walikwenda katika Nyumba za Michenzani na kusema aa! Sisi tulipewa na Mzee Karume, ndio alipewa na Mzee Karume na pengine alikuwa na nyumba yake na wala halipi kodi huyo, lakini amepewa nyumba na Mzee Karume sasa huyu lazima aji-*defend*, kwa sababu alikuwa na nyumba halipi kodi, lakini Mzee Karume kwa wakati ule amempa nyumba, kwa hiyo ile nyumba ni yake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kama tumepitisha sheria nyengine ya Kulipisha Kodi pamoja na mambo mengine baada ya mabadiliko ya sheria, basi sheria ndio ita-*apply* pale. Kwa maana hiyo, mambo yanabadilika kwa wakati na wala tusichukulie labda kwa nini, kwa sababu sisi hatukuchunguza mtu kwa awamu, isipokuwa tumechunguza matendo yake mtu aliyoyafanya. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka niendelee na hoja na kuja na jambo ambalo halijazungumzwa kuhusu kadhia ya Uwanja wa Ndege. Mhe. Spika, siku zote tunasema serikali fedha zipo tunaambiwa aa! Tunasema vile, kwa sababu sisi tunaona wakati unapotutuma kwenye Kamati unatuambia nendeni kachunguzeni, serikali itaiwezesha vipi, ili iweze kuwawezesha zaidi wananchi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mamlaka ya Uwanja wa Ndege ilikuwa kama Shamba la Babu, yaani kila mtu anajifanyia anavyotaka yeye. Tatizo kubwa zaidi Mhe. Spika na hili nafikiri ni jambo ambalo tujifunze sana, yaani ni bora mtu kukiri makosa yako kuliko kusema mambo ambayo si ya kweli na haya ndiyo yaliyotufanya tukaenda mpaka huko. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tulikwenda kule na kuwauliza wale wenye Mamlaka je, huu Uwanja wa Ndege kuna maeneo mangapi yaliyokodisha na kutupa idadi, basi tuliwaambia twende eneo moja baada ya jengine. Mhe. Spika, kuna maeneo mengi karibu manane wala hayana mikataba, hayalipi kodi. Hivi huu ni uwanja wa ndege, kwa sababu Uwanja wa ndege unatakiwa sehemu iwe *safe and security*, sasa hakuna mikataba na watu wanajifanyia wanavyotaka, yaani imekuwa kama Shamba la Bibi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, haya ndiyo tuliyokuwa tukiyasema, sasa yale tuliyoyazungumza na ndio maana tukasema haya ndiyo maradhi, tunaipa serikali ikayakague. Kwa kweli pale uwanja wa ndege kuna maeneo mengi ambayo yamekodishwa, kwanza tumekuta mikataba yote imeshamaliza muda, lakini bado watu wanaendelea na biashara na kuna wengine hata hiyo mikataba hawana na wapo uwanja wa ndege na wanafanyakazi.

Lakini baya zaidi Mhe. Spika, uongozi wenyewe wa Mamlaka unahusika moja kwa moja. Kwa mfano, leo Mkurugenzi wa Mamlaka anamiliki hanga, analipishwa na serikali dola 200 kwa mwezi na yeye anakodisha dola 1,000 kwa mwezi na huyo ndiye Mkurugenzi wa Mamlaka. *(Makofi)*

Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema Ikulu ni pahala patakatifu na wala sio sehemu ya kufanyiabiashara. Sasa mwalimu Nyerere aliposema Ikulu hakuwa na maana sio kule Ikulu, isipokuwa Ikulu ni ofisi yoyote aliyokukabidhi Mhe. Rais, maana yake kiti kile umekikalia kwa niaba yake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunaomba sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, bora tupige makofi kwa utaratibu, ili tuweze kumsikia Mhe. Mjumbe.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, tunaomba kwamba Ikulu kunafanywa biashara na wala siku kule Mnazimmoja aa! Ni uwanja wa ndege, kwa sababu Mhe. Rais kwa mujibu wa Katiba nyadhifa zote hizi ni zake. Kwa hiyo, ina maana Mamlaka ya Uwanja wa Ndege panafanywa biashara na Mkurugenzi. Sasa serikali iamue moja aidha Mkurugenzi aendelee kubakia na Ukurugenzi wake au Ukurugenzi atupishe aendelee kushughulikia hanga lake. *(Makofi)*

Vile vile sio hivyo tu pia Mkurugenzi anatumia mamlaka yake vibaya. Mhe. Spika, sisi baada ya kuwaita wale vijana kwenye Kamati na kuwahoji, basi kuna kijana mmoja ambaye anafanyakazi kwenye Kampuni yake ya *EROTACH* amemsimamisha kazi na alimwambia sikurudishi mpaka itakapotoka Ripoti ya Kamati Teule. Mhe. Spika, hii kweli ni haki? Kweli watu wanatumia mamlaka yao vizuri? *(Makofi)*

Mhe. Spika, jana Mhe. Salmin Awadh Salmin ambaye ni Mnadhimu wangu wa CCM alizungumza vizuri Katiba ya CCM inavyoeleza kwamba mtu atatumia mamlaka yake kwa mujibu wa Katiba, ndugu yangu Mhe. Ussi Jecha Simai pamoja na wengine Mhe. Ismail Jussa Ladhu wamenukuu Katiba, kwamba mtu hatotumia mamlaka yake vibaya ndani ya Katiba hii ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ndio maana masuala haya mengi jawabu yake yamo ndani ya Katiba na Mhe. Ali Salum Haji hakuchukua muda mwingi, lakini kila suala anasoma Katiba kifungu fulani. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunaomba watu wanapopewa mamlaka basi wasitumie mamlaka zile kwa kuwanyanyasa vijana wetu au wananchi wetu. Mhe. Spika, maana ya kuundwa Baraza la Wawakilishi ni kusimamia Haki za Wanyonge au Wananchi ambao wao hawana Wakurugenzi, Makatibu Wakuu, Mawaziri wala nani, yaani wao wanyonge tu ndicho tunachokizungumza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hili tunaliomba serikali kwamba lazima tufanye maamuzi magumu na wala tusione tabu ndivyo kazi zinavyokwenda. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hapo hapo uwanja wa ndege unajua kila siku tunapokwenda watu wanatupa mambo mengi. Kwa mfano, hivi sasa ipo Kampuni nyengine pale inaitwa *Kipanga Group*. Mhe. Spika, hii namuomba mwenyewe Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kupitia kwako Mhe. Spika na wala hatutaki kuiundia tume aende akachunguze kuhusu hii *Kampuni ya Kipanga Group* inafanyakazi za ufyekaji.

Kwa hivyo, akaangalie idadi ya wafanyakazi wanaolipwa na uhalisia wenyewe na hii wala sitaki tuiundie tume tumeshachoka kuunda tume *diagnosis* hii hapa Mhe. Spika, hiki ni cheti. Kwa kweli tunapounda tume tunapoteza fedha za umma, basi haya mambo ambayo yanayoweza kuzungumzika haraka haraka na Mzee Karume alisema 'La Leo Lifanywe Leo'.

Mhe. Spika, tunaomba Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano akitoka hapa aende akaangalie Kampuni ya *Kipanga Group*, kwanza kiongozi wa *Kipanga Group* ni nani, ndiyo hayo tunayoyasema kwamba ukoo pale unaendelea uwanja wa ndege halafu mpaka katika masuala mengine. Kwa hivyo, hili nawaachia wenyewe na watalitatua wenyewe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka niende katika suala la ajira. Kwa kweli juzi tumepitisha Sheria ya Utumishi wa Umma. Mhe. Spika, kitu ninachosikitia udanganyifu na sio kama tunadanganywa sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, yaani mpaka serikali inaidanganya serikali yenyewe Katibu Mkuu Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano anamuandikia barua Katibu Mkuu Wizara ya Nchi (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujaza nafasi moja, mbili, tatu, nne, tano, kila nafasi imewekwa na sifa zake. Kwa hivyo, Katibu Mkuu Wizara ya Nchi (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, anajibu sawa nakupa nafasi hizi hapa.

Sasa matokezeo yake Katibu Mkuu Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ah! Zile nafasi alizoziomba sizo ambazo alizoziajiri. Kwa mfano, ukija kwenye sifa kwa kweli watu wamefanya udanganyifu sana. Mhe. Spika, tunaomba hiki cheti serikali ikakifanyie kazi na wala sisi hatuna chuki na mtu, kwa sababu wale wote ni vijana wa Kizanzibari. Kwa hivyo, sisi kama tulivyosema hatujali kwamba aliyeajiriwa ni mtoto wa Mkurugenzi au Katibu Mkuu ama Waziri, lakini je sifa anazo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuna vitu vya aibu niviseme kwa mfano kuna mtu ameajiriwa kwa sifa ya *Form IV* na tumemwambia andika *statement* moja tu, mimi jina langu fulani bin fulani alilia, yaani hajui tena pamoja na cheti cha *VETA*, kusoma na kuandika hajui *diagnosis*. *(Makofi)*

Mhe. Spika, jengine kuna mfanyakazi mmoja Pemba huyu aliajiriwa kama sehemu ya Masjala, yaani ile kazi anayotumwa hajui anafanya nini, aliondolewa katika sehemu ile akapelekwa kwenye ulinzi hajui anafanya nini, amepelekwa uwanja wa ndege kukata majani.

Mhe. Spika, kijana huyo akilikamata *slasher* mpaka umwambie basi, jamaa kule anatuambia yule muombeeni aondolewe uwanja wa ndege kwa sababu atakuja kukata majani mpaka ndege unakuja. Kwa kweli watu wanaajiriwa hakuna vyeti na hali ya ajabu. Kwa hivyo, serikali ikachunguze haya ndio tuliyoyakuta. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye suala la Misali. Mhe. Spika, tusiambiwe kwamba labda tunao utashi au vipi, kwa sababu mimi ni Mwenyekiti wa Kamati inayosimamia masuala ya mazingira. Kwa hivyo, Idara ya Mazingira Pemba wakati tunapokwenda kutaka kusimamisha baadhi ya maeneo ya ujenzi, tunaambia Waheshimiwa mnasimamisha maeneo mbona hamchukui vigezo.

Mhe. Spika, Hoteli ya Misali tukitaka tusitake imekiuka sheria zote, kwa sababu kwanza sisi tumeona *lease* imetolewa, lakini *lease* iliyotolewa ilitolewa zaidi mwaka, kwa sababu mwanzo walikuwepo pale akinamama ambao wanaopanda miti na walipimiwa eneo lile kwa ajili ya kuandikiwa lease, kwa ajili ya kuhifadhi ile miti yao, ili pale wanapolima wapate kuvuna, lakini baadaye wakaja wakenda wajanja wachache.

Mhe. Spika, eneo hili wale akinamama tuliwaita na kutueleza kweli wamelipwa shilingi milioni 10. Lakini yule ambaye aliyewalipa shilingi milioni 10 amekiuka sheria zote za nchi, kwa sababu kwanza eneo lile halina hata mita moja ambayo inayoruhusiwa kujengwa kisheria, kwani eneo lenyewe lipo baharini, yaani sehemu yenyewe kama kisiwa na wala haifiki mita 30 kutoka katika ufukwe wa bahari yanapoishia maji ukipima mbele na nyuma kwa sababu eneo lenyewe ni dogo. Mhe. Spika, eneo lile limejengwa bila ya utaratibu. *(Makofi)*

Lakini baya zaidi Mhe. Spika yaliwahi kupelekwa maombi *ZIPA* na raia wa kigeni wa Canada. *ZIPA* walisema eneo hili la Misali, yaani ile Wesha yote tumezuiliwa na serikali tusitoe Kibali cha Uwekezaji wa aina yoyote, kwa sababu wale walipeleka maombi ya kutengeneza ile *Diving*, yaani anajenga banda dogo hivi na viboti vyake vya kuzamia.

Mhe. Spika, *ZIPA* wametuambia kwamba wamepewa agizo na serikali kuwa kuna maeneo serikali wameya-*reserve* kwa ajili ya utafiti na uchimbaji wa mafuta. Kwa hivyo, eneo lote la Misali haliruhusiwi uwekezaji wa aina yoyote. Mhe. Spika, maneno haya si ya kwangu, isipokuwa ni maneno ya watendaji wa serikali tena Ofisi ya *ZIPA* Pemba, eneo la Misali ni kwa ajili ya utafiti na uchimbaji wa mafuta. *(Makofi)*

Sasa eneo hili Mhe. Spika tayari watu wanalimiki na wameshajenga hoteli na tulisema hoteli yenyewe imekiuka sheria zote. Je, leo mafuta yamepatikana eneo la Misali Wesha, sasa wale wamiliki wa hoteli ile itaambia nini, *share holder* wamendikwa humu na mimi wala sitaki kuwataja, kwa sababu Ripoti ya Kamati imeeleza *share holder*. Mhe. Spika, ina maana hapa kuna watu tayari wameshawekeza kwa *future*, yatakapokuja kupatikana mafuta na serikali waka-*negotiate* na watu waliovunja sheria. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunapozungumza haya mambo kwanza tuliangalia taratibu za mazingira zimekiukwa, tukaja katika hali ya matenki ya mafuta ni tatizo. Lakini baya zaidi eneo lile limekuwa *reserved* kwa ajili ya *petroleum exploitation*. Sasa haya tuyaangalie kwa ajili ya baadaye na wala tusiyaangalie hapa.

Mhe. Mkuu wa Mkoa tuliwahi kupata taarifa kwamba alizuia, lakini ndio yale aliyozungumza yule mwekezaji alisema ah! Nilimtuma mtu wangu na alikwenda pale na mambo yakamaliza. Sasa haya ndio tunayoyazungumza kwamba hiki ni cheti na serikali ikakifanyie kazi. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, zingatia muda.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, sawa namalizia. Sasa nizungumzie kuhusu *generator*, mimi naona tabu sana kwa sababu ilipokuwa inapitishwa baadhi ya hii miradi sisi wengine tulikuweko huko. Serikali iliporuhusu fedha za *MDRA* kutatua matatizo ya dharura ambayo serikali kidogo inakuwa magumu kwake, Fedha za Msamaha wa Madeni. Kwa kweli fedha hizi ni mbaya sana, kwa sababu ni kodi ya wenzetu wanaotuonea huruma kwa umasikini wetu na kutuletea sisi fedha zile.

Mhe. Spika, *generator* limenunuliwa na Wizara ya Fedha na kuletwa pale uwanja wa ndege, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha anamuandikia Katibu Mkuu Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano nimeshakuletea *generator* tena ni *standby generator*, yaani umeme wakati wowote ukija kuleta shoti, basi *generator* lile lifanyakazi, kwa ajili ya huduma za uwanja wa ndege.

Kwa hivyo, *generator* lime-*cost* karibu shilingi milioni 300 fedha za wahisani ambao wanaotuonea huruma, pia *warrant* wake wa *guarantee* ni mwaka mmoja. Sasa yule *supply* ndani ya mwaka mmoja alitakiwa alifanyie *installation* na kama atalifanyia *installation* ndani ya mwaka mmoja ikiwa kuna hitilafu yoyote itakuwa ni juu yake.

Mhe. Spika, *warrant* ya *guarantee* ya mwaka mmoja umepita na Makatibu Wakuu hawa wanajua kwamba *warrant* ule ukeshamaliza inabidi suala lile serikali italibeba wenyewe. Kwa kweli hivi sasa ni sawa kama tumeuziwa jini, kwa sababu *generator* ile mpaka leo hatulijui kama ni bovu au zima. Kwa hiyo, ina maana serikali itoe fedha zaidi ya shilingi milioni 75 kwa ajili ya kulifanyia *installation*, kwa ajili ya kulijaribu ili kujua kwamba linafanyakazi au halifanyikazi *are we serious*? *(Makofi)*

Kwa hiyo, ndipo pale tunaposema kwamba fedha zipo, lakini mipango ya matumizi ya fedha hatuna. Sasa Mhe. Spika, hili tunaomba sana kwa sababu serikali humu tumewapa mambo mengi, lakini kuna baadhi ya mambo tunaomba sana Mhe. Spika, serikali iyafanyiekazi kwa haraka.

Kwa mfano, kama hili la *generator* tuliitaka serikali basi angalau ndani ya mwaka mmoja watafute fedha popote aidha kwenye hiyo Mamlaka ya Uwanja wa Ndege au Wizara yenyewe ya Miundombinu na Mawasiliano ama Wizara ya Fedha, kwa ajili ya kufanyiwa majaribio *generator* lile, ili lijulikane kama ni zima au bovu. Mhe. Spika, hali hii ndio kuokoa fedha za umma.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, nataka umalizie, kwa sababu yote unayoyasema ni marejeo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru baada ya kunipa nafasi hiyo, lakini kama nilivyosema kwamba nia yetu ilikuwa ni njema tu, kujaribu kuzungumza na serikali kuangalia kuna matatizo gani. Kwa hivyo, ninaamini serikali kwa sababu wakati tunazungumza wakao kimya wanatusikiliza na wengine wanaandika.

Kwa maana hiyo, naamini haya watayachukua na kwenda kuyafanyiakazi, pia naamini kwamba serikali itakuja na ripoti nzuri, ambayo itaturidhisha sisi Wajumbe wa Kamati, Wajumbe wote wa Baraza na wale wananchi waliotupa taarifa pamoja na wananchi wote wa Zanzibar.

Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi. Pili tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uwezo wa kutukutanisha tena asubuhi hii ya leo.

Mhe. Spika, naomba nikupongeze kwa namna ambavyo unaendesha shughuli zetu za Baraza kwa misingi ya kidemokrasia mikubwa sana. Vile vile niwapongeze Wajumbe wako wa Baraza kwa michango yao ambayo kwetu inaleta sura mpya ya kuimarisha demokrasia na maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, pia niwashukuru wajumbe wa kamati teule kwa kazi waliyoifanya na wakaweza kutuwasilishia ripoti hii mbele ya baraza lako tukufu, serikali yetu nia na dhamira yake ni kupampbana na kila kitendo kiovu, kupambana na ubadhirifu, kupambana na rushwa na lile lote ambalo halina maslahi kwa nchi yetu basi serikali yetu imejipanga kupambana nalo, serikali haina nia hata kidogo kunyanyaza mtu yoyote ama kumbagua mtu yeyote kwa misingi yoyote ile. Nia yetu ni kujenga serikali yenye uadilifu, yenye maadili, yenye dhamira njema iliyo tayari kuwatumikia wananchi wetu.

Mhe. Spika, taarifa hii ya Kamati Teule ya Baraza kwangu mimi niseme naunga mkono jitihada za serikali katika kuimarisha maadili ndani ya serikali na ndani ya nchi yetu, kwa nini nasema hivyo kwa sababu tarehe 11 Novemba, 2010 wakati Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alipofanya uzinduzi wa baraza lako la nane la Baraza la Wawakilishi, alisema mambo yafuatayo naomba nimnukuu.*(Makofi)*

"*Mhe. Spika, katika kutekeleza utawala bora maadili ndio ajenda ya kitaifa suala hili linawahusu viongozi waliochaguliwa, walioteuliwa na watakaoteuliwa baadae ili wawajibike kwa wananchi waliowachagua, lakini pia maadili yanawahusu wananchi wote. Rushwa ni suala moja linaloharibu maadili ya viongozi watumishi wa serikalini na wananchi kwa jumla tutapambana na rushwa kwa hali yoyote na hatua moja kubwa tutakayoichukua ni kuimarisha sheria zetu na mfumo mzima wa kupambana na rushwa".*

Mhe. Spika, Mhe. Rais aliendelea kusema yafuatavyo naomba niyanukuu.

"Katika kipindi cha miaka mitano ijayo serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar awamu ya saba yenye muundo wa umoja wa kitaifa itaendeleza jitihada za kukuza demokrasia na utawala bora, serikali yangu itazingatia utawala bora wenye kuheshimu sheria haki za binaadam, uhuru wa wananchi kutoa maoni ya kujieleza na ikajali usawa pasipo ubaguzi wa aina yoyote iwe kwa sababu ya itikadi za chama, dini au eneo analotoka mtu".

Mhe. Spika, napenda niyaseme haya kuonyesha kwamba serikali hii inayoongozwa na DK. Shein nia na dhamira yake ni kutenda uadilifu, kutenda haki na haina nia hata kidogo kumbagua yoyote ama kuona kwamba fedha au mali ya serikali inapotoea, Nia yake ni kujenga serikali iimara itakakayotumikia wananchi kwa mashirikiano makubwa.. Lakini Mhe. Spika, lazima tuelewe kwamba serikali ni system na systerm ni *process* . Katika jitihada zetu za kuleta mabadiliko na mabadiliko yenyewe ni process, kwa hivyo kila kila hatua

zitaendelea kuchukuliwa na tuamini nia ni hiyo lakini tujue kama ni *process* lazima tutaanza hatua moja, kwenda hatua nyengine lakini nia yetu ni kufikia hatma njema kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mhe., Spika, kutokana na maelezo hayo ya rais na kutokana na utaratibu mzima wa nia njema ya serikali napenda nilihakikishie baraza lako tukufu kwamba tutachukua kila hatua kuhakikisha kwamba nyumba yetu iko safi. Lakini jambo kubwa Mhe. Spika, katika kutenda hiyo ni lazima misingi ya haki izingatiwe maana uongozi ni kuhakikisha haki inatendeka kwa kila mmoja wetu. Tukitenda haki usawa na umoja utakuwepo. *(Makofi)*

Kwa hivyo Mhe. Spika, hatua zetu zote tutakazochukua tutahakikisha kwamba haki ya kila mmoja wetu inapata nafasi yake, nataka niwahakikishie baraza lako tukufu kwamba serikali yetu ni sikivu na iko tayari ku kusikiliza, na iko tayari kuwatumikia wananchi kwa misingi ya uadilifu wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, yapo malalamiko yaliyotolewa na Waheshimiwa wajumbe hapa kwamba baadhi ya watendaji wetu ima wanapoitwa na kamati, ima wanapotakiwa kushiriki kwa njia moja au nyengine katika vikao maalum vya kamati huwa hawaitikii wito huo. Mhe. Spika, tuliwahi kutoa utaratibu katika baraza lako tukufu hili na leo napenda niurudie tena kwamba watendaji wote wa serikali wafuate taratibu kwa kuitikia wito wa kamati wanapoitwa ndani ya kamati zetu, tuheshimu Baraza la Wawakilishi, tuheshimu kamati za Baraza la Wawakilishi maana hiyo ndio misingi ya kuweka demokrasia iliyo wazi. Tujenge misingi ya haki ili tuheshimu sana maoni ya wananchi wetu na tuheshimu maoni ya wawakilishi wa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, serikali imepokea maoni imepokea ripoti na kumbu kumbu zake ambazo ndizo vielelezo vya ushahidi, ripoti hii imegusa maeneo mengi makubwa na ambayo yanahitaji serikali kuyafanyia kazi kwa undani, kwa uadilifu na haki ili uamuzi umfurahishe kila mmoja. Ili wananchi wetu waridhie kuona kwamba baraza hili na serikali yake imekusudia kutenda haki bila ya kubagua mmoja wetu.

Maendeo ambayo ripoti hii imeyagusa yamehusu taratibu za matumizi ya fedha, yameuhusu mambo ya umiliki wa ardhi, yamehusu mambo ya uwanja wa ndege, yamehusu fidia za mali walioathirika, yamehusu mikataba, yamehusu sekta binafsi, yamehusu ununuzi wa jenereta la *Air port*, yamehusu utaratibu wa ajira Uwanja wa Ndege, yamehusu uvamizi wa fukwe, yamehusu uharibifu wa mazingira, yamehusu mikataba ya nyumba za SMZ, yamehusu uhaulishaji wa majengo, yamehusu ukodishwaji wa kisiwa cha Changuu, yamehusu majanareta ya usambazaji wa maji na mengineyo.

Mhe. Spika, nyote mtaamini kwamba kazi hii ilikuwa kubwa na iliwachukua muda mrefu sana wajumbe wa kamati teule kuifanyia kazi mpaka kuja na ripoti hii, kwa hivyo kwa vyovyote vile itakavyokuwa na serikali kwa upande wake itabidi ifanye kazi kubwa ya kuipitia moja baada ya moja, ili iweze kuleta taarifa yake mbele ya baraza hili tukufu ambayo nina hakika kabisa itakidhi mahitaji ya wajumbe wako wa Baraza hili.

Mhe. Spika, kutokana na ukubwa wa ripoti yenyewe na kwa sababu hata kanuni zetu zinatutaka tunapowasilisha ripoti basi na zile kumbu kumbu sa ushahidi ziende sambamba na ripoti hiyo, kwa sababu kumbu kumbu hizo za ushahidi ukweli kutokana na ukubwa wake tulizipata jana na hizo kumbu kumbu za ushahidi Mhe. Spika, ndizo zitakazotusaidia katika kutoa maamuzi ya haki. Kwa hivyo ningeliomba sana baraza lako tukufu liridhie kuipokea ripoti hii kwa ujumla wake pamoja na kumbu kumbu hizo zenye vielelezo ili tuweze kuzifanyia kazi, kwa sababu ukiangalia sisi wajumbe wako wa baraza lako tukufu kwa upande mmoja ndio tulioibua hizi tuhuma baada ya kusikia maelezo kwa wananchi mbali mbali au watendaji mbali mbali na mambo mengine. *(Makofi)*

Lakini sisi sisi tuliofanya kazi hii ya ushahidi kutafuta taarifa hizi, lakini ni sisi sisi ndio tutakaotoa hukumu hizi, kwa hivyo bila ya kupata ushahidi wa kutosha na tukafikia kipengele baada ya kipengele hatutoweza kufanya uamuzi wa busara na uamuzi wa haki. Hivyo naliomba sana baraza lako hili badala ya kupitia kipengele kwa kipengele tuichukue ripoti kwa ujumla wake tukaifanyie kazi na baadae tuiwasilishe taarifa hiyo hapa katika baraza lako. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tumesema hapa sisi baraza hili ni ngome ya wananchi kwa hivyo kuendelea kwetu kuwa ngome lazima kuhakikisha haki inatendeka kwa watu wote, maana ngome hilo nataka nilihakikishie baraza lako tukufu kwamba kazi hii tutaifanya kwa uadilifu mkubwa na umakini wa hali ya juu ili tulete taarifa iliyo sahihi, na mimi naunga mkono muda ambao Kamati Teule imetupa katika kipindi cha miezi mitatu nina hakika kabisa tutaweza kuifanya kazi hii vizuri sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa hivyo nitaliomba sana baraza lako tukufu liridhie suala hilo ili tuende kuifanyia kazi tipoti hii nakuhakikishia kwamba serikali yetu ni sikivu na iko tayari kufanya kila juhudi kuhakikisha maadili na uadilifu yanalindwa, lakini kabla ya kumalizia naomba nitanabahishe kitu kimoja. Ni lazima tujenge mazingira ya

kuheshimu sana viongozi wetu hawa wa juu wa kitaifa hususan Marais wetu, vile vile tusiwasahau marais waetu wastaafu mzigo wa kazi ya urais ni mkubwa sana, ni ngumu sana, nzito sana. Viongozi wetu wastaafu hawa wanafanya kazi ya kututumikia katika kipindi kigumu sana na wanakuwa na nia njema sana ya kuitumikia nchi yao.

Mhe. Spika, mpaka ukisikia kuchaguliwa kuwa rais mchakato wake ni mzito na mkubwa sana, kwa hivyo kwa maana moja au nyengine nasema viongozi wetu tunaowapata kutuongoza wanakuwa ni waadilifu sana na makini sana, kwa hivyo inapofikia wakati wa kustaafu wakapumzika lazima tuwasaidie viongozi wetu hawa wapumzike kwa salama na tupunguze baadhi ya mambo ambayo yanawavunja moyo na kuwasononesha na kuwaweka katika hali isiyo na furaha. Ni vizuri sana tunapofanya maamuzi wetu tukawafikiria viongozi wetu hawa maana wamesaidia sana katika kujenga nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya kusema maelezo hayo naomba niseme kwamba serikali imeipokea ripoti yetu hii, nataka kuwahakikishia kwamba kipengele baada ya kipengele tutakifanyia kazi na tulete majibu yaliyo sahihi na yenye kutenda haki kwa watu wote. Ahsante sana Mhe. Spika, *(Makofi)*

Mhe. Omar Ali Shehe (Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi) Mhe. Spika, awali ya yote naomba nitumie fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuja mbele ya baraza lako tukufu kwa lengo la kufanya majumuisho ama kufunga mjadala huu ambao ulianza juzi tarehe 18/04/2012.

Mhe. Spika, kazi hii ya kamati teule takriban iligusa maeneo ama wizara kama tulivyozifanyia kazi kwa mujibu wa hadidu rejea tulizopewa, lakini nadhani ingelikuwa ni busara sana kwa sababu yale tuliyoyaona takriban yanagusa serikali nzima, kwa msingi huo ingelikuwa ni vyema sana na mara nyengine nashauri kwa mambo kama haya ya kitaifa serikali yote ingelikuwepo hapa pamoja na watendaji muhimu, ili aliyegusa akapata kuona alivyoguswa na yule ambae hakuguswa basi akapata fursa ya kuona mwenzake alivyoguswa ili iwe ni mfano wa utendaji uliotukuka katika serikali. Kwa hivyo leo ingelikuwa ni siku muhimu sana kwa mawaziri pamoja na watendaji wakuu wa taasisi zetu kuwepo ili kuona hali halisi inavyokuwa katika serikali ili iwe ni muongozo wa taasisi zao katika siku zinazovyokwenda.

Mhe. Spika, kamati yetu teule imechangiwa takriban na wajumbe ishirini na nne (24) naomba kwa heshima na taadhima uniruhusu niwatambue wajumbe hao ambao walichangia ripoti yetu.

1 Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2. Mhe. Ali Salum Haji
3. Mhe. Abdi Mossai Kombo
4. Mhe. Ussi Jecha Simai
5. Mhe. Hassan Hamad Omar
6. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
7. Mhe. Salehe Nassor Juma
8. Mhe. Farida Amour Moh'd
9. Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak
10 Mhe. Abdalla Moh'd Ali
11. Mhe. Subiet Khamis Faki
12. Mhe. Mohammed Haji Khalid
13. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
14. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
15. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
16. Mhe. Rashid Seif Suleiman
17. Mhe. Sulaiman Hemed Khamis
18. Mhe. Mussa Ali Hamad
19. Mhe. Salmin Awadh Salmin
20. Mhe. Hijja Hassan Hija
21. Mhe. Asha Bakari Makame
22. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
23. Mhe. Hamza Hassan Juma
24. Mhe. MohammedAboud Mohammed

Mhe. Spika, takriban wajumbe wote waliochangia wamesifu kazi nzuri sana iliyofanywa na kamati, nami kwa niaba ya wajumbe wa kamati naomba nizipokee pongezi hizo au salamu hizo na nizirejeshe tena kwa

waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa sababu wao ndio walioikabidhi kamati kazi, kwa hivyo kama ni sifa tunaomba Mhe. Spika, zirudi kwa wajumbe kupitia kiti chako. *(Makofi)*

Lakini mbali ya pongezi waheshimiwa wajumbe kikubwa walichochangia ilikuwa ni kusisitiza utendaji na utekelezaji wa mapendekezo yaliyomo kwenye ripoti ya kamati, waheshimiwa wajumbe walisisitiza sana uwajibikaji katika sekta za umma hayo takriban ndio yaliyokuwa mchangio kwa waheshimiwa wajumbe. Baadhi ya wajumbe waliomba ufafanuzi wa baadhi ya mambo, ulihitajika ufafanuzi wa suala zima la ukodishwaji wa jengo la Mambo Msige Mhe. Mbarouk jana pamoja na baadhi ya wajumbe wa kamati walinisaidia kulitolea ufafanuzi suala hilo, nami kwa sababu ripoti kamili au maelezo kamili yamo kwenye ripoti na kwa kuwa baadhi ya wajumbe wa kamati wamenisaidia naomba tukubaliane na maelezo yaliyomo katika maelezo.

Lakini vile vile ufafanuzi wa namna ya tatizo la ajira na namna wizara mbili zilivyotupiana mipira ama zilivyokingiuka ama kila mmoja alivyokingika waheshimiwa wajumbe wa kamati nawashukuru sana wamenisaidia sana katika michango yao. *(Makofi)*

Lakini vile vile kulikuwa na ufafanuzi ulihitajika namna serikali inavyopaswa kuwasaidia vijana waliojikusanya Air Port, Mhe. Hamza Hassan Juma asubuhi hii kanisaidia katika dhamira ya kamati kusema vile kwamba tunaiomba serikali iwatafutie misaada vijana wale ili wajiendeleze. Kwa hivyo na hili Mhe. Spika, nadhani inatosha nikubaliane na waheshimiwa wajumbe kwamba ufafanuzi ni kama ulivyotolewa na Waheshimiwa wajumbe, lakini kama tutapata muda mzuri zaidi wa kuisoma ripoti na kuangalie vielelezo maelezo yatatusaidia sana katika kufikia adhma hiyo.

Mhe. Spika, kamati imeshatekeleza wajibu wake baraza mlitutuma na sisi tukafanyakazi na kazi yetu ni kuchnguza na tumechunguza, kazi yetu nyengine ilikuwa ni kuandika ripoti tumeandika ripoti, kazi nyengine ilikuwa kutoa mapendekezo na mapendekezo tumetoa. Kwa msingi huo leo tunatua kazi au tunatua mzigo mliotutuma au mzigo mliotupa, kama ingelikuwa ni uchezaji mpira basi tungelisema sasa mpira umeondoka katika goli letu, sasa mpira uko katika goli la serikali.

Mhe. Spika, kazi haikuwa rahisi hata kidogo tumefanya kazi katika mazingira magumu sana sana kabisa ya kugombana ya kususiana ya kufika mpaka kutoleana maneno lakini yote hayo kwa kweli ilikuwa kwa lengo moja tu , kwa lengo la kutekeleza wajibu ambao taifa limetutuma. Mimi nachukua fursa hii kujipongeza binafsi maana nikisubiri kupongezwa nitachelewa, kawaida ya sasa kwanza raha ujipe mwenyewe ujipongeze mwenyewe. Mhe.Spika uenyekiti wa kamati hii ulikuwa ni mgumu sana maana mbali ya watendaji lakini wakati mwengine hata baadhi ya wajumbe wangu tulikuwa tunakosana, wakati mwengine unataka kwenda huku mtu anakuelekeza huku, jazba wakati mwengine inapanda lakini kwa umakini wa mwenyekiti umwambie hapana turudi kwenye mstari. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kazi mliyotutuma ni kazi ya watu sio kazi ya watu watano lakini kazi ya watu wote, wajumbe wa baraza wametuamini wametupa kazi kwa hivyo lazima turejeshe imani wao wana akili na kuna siku tutakwenda mbele ya baraza ripoti itajadiliwa, tusije tukafika pahala mbele ya kadamnasi ya watu tukadharaulika twendeni katika mstari huu. Na taka niwaambie kuna mambo mengi sana na mtu anayetaka Mhe. Spika, kama utaniruhusu niwaonyesha kuna mambo mengi sana ambayo yalitakiwa yaingizwe lakini nikawambia hapana hatukutumwa hivi tulichotumwa ni hichi.

Mhe. Spika, kwa hivyo najipongeza binafsi kwamba tumefanya kazi na kazi ambayo imetukuka imeambatana na uaminifu na uadilifu wa hali ya juu, kwa sababu siku zote nilisema sitaki nitumike au hatutaki tutumike kumdhulumu mtu siku moja tutakwenda kujibu, kupata machungu mtu kwa sababu ya sisi kwa kitu ambacho hajafanya haiwezekani. Kwa hivyo nataka nilihakikishie baraza lako kwamba tumefanya kazi kwa mazingira magumu lakini zaidi uaminifu na uadilifu kwa kweli ndio uliotuongoza, naamini kwamba ripoti yetu imelenga katika haki.

Kamati yetu ingelikuwa na uwezo wa kwenda na kuripoti kila kitu tungelikuwa na uwezo wa kusema hivyo kwamba kila kitu safi tu, lakini tungelifanya hivyo sijui baraza lingelituona je, kila kitu *Air Port* safi, kila kitu huko kwengine safi sijui nyie mngelituona je baadae na sijui wananchi wangelituonaje. Kwa hivyo Mhe. Spika, nataka niseme hivyo, naomba nitumie nafasi hii kuipongeza kwa dhati serikali na msimamo wa serikali leo umetolewa na Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwamba serikali itakaa kitako na kuifanyia kazi ripoti hii. Kwa hivyo tunapongeza kwa sababu mwisho wa kazi nzito ambayo imeligharimu taifa wananchi sasa hivi wanasubiri kuangalia nini kitatokea baada ya hapa, kwa hivyo sisi kama kamati tunalipokea hilo na sasa tunasubiri serikali ikae na iifanyie kazi ripoti yetu.

Mhe. Spika, naomba nikumbushe tu kwamba sote tuna wajibu wa kufahamu kwamba wakati umebadilika sasa na kama wakati umebadilika maana yake na sisi wenyewe tunapaswa tubadilike, maana kusubiri wakati utubadilishe itakuja kuwa ni tatizo ni afadhali tubadilike tu sisi wenyewe. Muamko wa wananchi wetu sasa hivi kwa kweli ni mkubwa sana. Mimi namshukuru sana Mhe. Saidi Ali Mbarouk (Waziri wa Habari) juzi baada ya kutoka nje alinambia kesho nawaita watendaji wangu. Kweli kupitia vyombo vya habari nilimuona kazungumza na watendaji wake kuwambia jamani mambo yamebadilika. Mhe. Saidi nakupongeza sana.

Mhe. Spika, tunawajibu wa kufahamu wote kama msingi wetu ni watu (wananchi) kwa mujibu wa katiba yetu ibara ya 9, msingi wa kuwepo kwetu hapa ni watu. Mhe. Raisi asingelikuwepo kama si watu, Mhe. Spika, wewe umekuwepo kwenye kiti hicho ni kwa sababu ya wawakilishi ambao wamechaguliwa na watu, Waheshimiwa wawakilishi tupo tunazunguka na viti kwa sababu ya watu, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na Watendaji mbali mbali kwa sababu wameteuliwa na mtu ambaye kachaguliwa na watu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, hatuna budi turejeshe hashima kwa watu. Lazima tuwaheshimu wavua kombe, lazima wauza madafu tuwaheshimu, waokota mpeta lazima tuwaheshimu. Mhe. Spika, wanaofyeka majani lazima tuwaheshimu, wanaochuuza na kuvua lazima tuwaheshimu. Huo ndio msingi wa utawala wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, narudia kusema kwamba Kamati imekamilisha ripoti yake, ripoti tumeikabidhi, tumekabidhi vielelezo, lakini vile vile tumakabidhi hansard kwa yule ambaye atahitaji kupata maelezo yanayotokana na kauli.

Mwisho kabisa naomba nimalizie kwamba kazi hii imefanywa na wanadamu, wanadamu wenyewe ni akina Omar Ali Shekhe na Mtando kazi iliyotukuka na iliyokuwa haina makosa ni moja tu, ni kazi ya Mwenyezi Mungu. Natangulia kuomba radhi kwa lolote litakalotokea kama ni kosa tulilolifanya katika kazi yetu. Hatukufanya kwa utashi tulifanya kwa lengo la kutumikia taifa letu Mhe. Spika, (*Makofi*)

Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Zanzibar.
Mhe. Spika, nakushukuru Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa kwamba sasa ripoti hii tuipokee pamoja na mapendekezo yaliyomo. Nilikuwa namsubiri Mhe. Mwenyekiti, aseme kitu kimoja muhimu sana ambacho Waheshimiwa Wajumbe mlikichangia na kwa kweli kina umuhimu wa pekee. Katika maelezo yake ya mwisho alisema kwamba binaadamu ana udhaifu wake, mengine yanaweza mtu yakampitikia.

Mtakumbuka kwamba katika mapendekezo mbali mbali ambayo yamo katika muhtasari huu pamoja na ripo yenyewe. Michango iliyotoka ndani ya Baraza hili kwa baadhi ya waheshimiwa wajumbe ni kwamba pale ambapo pana mapendekezo ya kukatisha mikataba basi serikali izingatie sana ukatishaji wa mikataba hiyo isije ikatuletea hasara kubwa zaidi. Hili ni jambo muhimu sana na ambalo linapaswa kuingia katika ripoti hii kuwa ni sehemu ya ripoti. Mifano yake imetokea pale Bungeni, kuna mikataba ilikatishwa, ilivunjwa kupitia uwamuzi wa Bunge, hasara yake ilikuwa ni kubwa mno na kwa kweli mpaka leo hii hatuna hakika ilifikia wapi. Kwa hiyo na humu kuna mapendekezo ya aina hiyo ambayo yalipendekezwa na Kamati yetu hii. Ripoti ambayo inaonekana kwa mazingira kwamba tunaikubali sote wajumbe wa upande wa back bancher na serikali pia.

Hili nalo liingie kuwa ni sehemu ya ripoti hii kabla sijawahoji ili serikali inapokea kazi hii inakwenda kuitekeleza ikielewa kwamba kuna maelekezo kwamba inapotokezea pahala pameambiwa na mapendekezo haya kwamba mkataba uvunjwe basi tuzingatie matokeo ya kuvunja huko je, haitoiletea serikali hasara iliyokubwa zaidi. Kwa sababu niya ilikuwa ni kutengeneza ili mambo yawe mazuri kwa faida ya wananchi, kuja kuongeza hasara hiyo itakuwa sio faida ya wananchi.

Nilitaka nilisema hilo na hilo ni jambo muhumu sana. Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe niwahoji wale wanaopokea na kukubali ripoti hii pamoja na mapendekezo na maelekezo mengine yaliyotolewa wanyanyue mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Ripoti inakabidhishwa kwa serikali pamoja na mapendekezo yake na maelekezo ambayo mmeyakubali, pamoja na vielelezo mbali mbali ambavyo vitasaidia. Kwa sababu katika ripoti hii kuna baadhi ya mambo yanahitaji kuchukuliwa hatua za kisheria. Vipo vyombo ambavyo kwa kawaida vinategemewa vifanye

kazi hiyo kwa hivyo vile vielelezo kwa ajili ya kufanya rejea mpaka kufikia kuchukua hizo hatua za kisheria inabidi wawe navyo visaidie katika kazi hiyo.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya hayo kabla ya kusitisha shughuli zetu hadi jioni kuna kazi mbili mliamua na mkatuachie tuzifanyie kazi. Tuliamua katika Baraza hili kwamba iwepo Kamati teule ya kuchunguza masuala ya Manispaa ya Zanzibar. Kamati teule hiyo nitaitangaza jioni Mwenyezii Mungu akipenda.

Pia hadidu rejea ambazo tumezipata kutokana na hansard pia nitazipitisha hapo jioni kwa mujibu wa Kanuni nadhani ni 118 inatakiwa zipitishwe na Baraza, hazitopitishwa na watu wawili, watatu, *quorum* inabidi itimie ndipo tuupitishe uwamuzi huo wa hadidu hizo kama tulivyozipata katika hansard. kabla ya kumuomba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kutoa hotuba na hoja ya kufunga mkutano huo.

Nilikuwa nataka nisema hivyo ili jioni tuje tena ikiwezekana mapema kwa sababu shughuli ya jioni siyo kubwa. Niwaombe Waheshimiwa Wajumbe tujutahidi kufika mapema, haitopendeza kuona wajumbe wanachelewa, ili tuifanye kazi hiyo na baadaye tumuombe Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, atoe hoja ya kufunga mkutano wetu huu.

Baada ya hayo machache Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni sana kwa mashirikiano ambayo tumekuwa nayo kwa Mkutano huu wa Saba ambao mara hii ni historia umekuwa ni mkutano mrefu sana. Umekuwa mrefu kwa sababu shughuli zilikuwa nyingi, Miswada sita ambayo ilijadiliwa, pamoja na ule wa saba ambao tulimalizia kazi iliyoachwa kwenye mkutano uliopita, ripoti za kamati saba, majadiliano ya shughuli mbali mbali za serikali ambazo zilibakia na ziliahidiwa kutolewa taarifa hapa.

Nyengine ni hoja, kauli za Mawaziri na hatimaye kazi hii tuliimaliza hivi punde.

Tulikuwa na shughuli nyingi, wananchi ni vyema wakajua kwamba kukaa kwetu kwa muda wote huo karibu wiki tatu imekuwa kwa sababu ya shughuli nyingi ambazo wananchi wenyewe walipaswa wafahamu nini kinachoendelea katika shughuli zetu za mkutano huu wa saba.

Baada ya hayo basi nisitishe shughuli hizi na kuahirisha kikao hichi hadi saa 11:00 jioni leo.

(Saa 5:10 Asubuhi Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tulikubaliana pale tulipoakhirisha kikao kipindi cha asubuhi kwamba jioni ya leo kabla ya kumkaribisha Mhe. Makamo wa Pili wa Rais nataka nifanye kazi moja ambayo Baraza mmenituma niifanye ya kuunda Kamati Teule kwa ajili ya kufuatilia masuala ya Manispaa.

Kamati Teule kwa mujibu wa kanuni ya 117 (1) inaeleza kama ifuatavyo:

Baraza linaweza kuunda Kamati Teule kwa ajili ya jambo fulani, kifungu kidogo cha (2) cha ibara hiyo. Kamati Teule itapendekezwa kwa njia ya hoja itakayotolewa na mjumbe na kuamuliwa na Baraza, taarifa ya hoja hiyo haitajadiliwa, Kamati Teule itakuwa na wajumbe wasiopungua watano (5) ambao watateuliwa na Spika. Mjumbe aliyependekeza kuunda kwa Kamati Teule atakuwa ni miongoni mwa wajumbe wa Kamati hiyo, lakini si lazima kuwa mwenyekiti wa kamati hiyo.

Waheshimiwa Wajumbe nilitaka nichukue kipengele hicho kazi ya kupendekeza Kamati Teule kwa njia ya hoja ilikwishafanyika ambapo Mhe. Asha Bakar Makame ndiye aliyetoa hoja hiyo na wajumbe mkaamua kwamba sawa hiyo Kamati Teule iundwe. Kwa hivyo, kwa mujibu wa kanuni hiyo ya 117 (2) kazi ya kuamua au kuunda hiyo Kamati Teule ni kazi ya Spika. Hivyo, chini ya ibara hiyo ninafuraha kutangaza hiyo Kamati Teule ambayo inaundwa kwa mujibu wa kifungu hicho.

Pia nataka Waheshimiwa Wajumbe muelewe kamati hii imetajwa kwamba iwe na wajumbe wasiopungua watano (5) kufuatana na mwenendo wa matumizi na shughuli nyingi zinazojitokeza hapa na pale, mara nyingi kama ilivyokuwa Kamati Teule ambayo tulimaliza ripoti yake kipindi cha asubuhi ilikuwa na wajumbe watano, tungeweza kwenda mpaka saba (7) kwa sababu *minimum* ndio hao watano. Waheshimiwa Wajumbe kwa kuzingatia hali ya kifedha na hii pia nimeamua tuteuwe wajumbe watano kama ifuatavyo:-

Wajumbe hawa nimewapanga si kwa sababu kwamba labda yule wa mwanzo ndie mwenyekiti, kanuni hiyo inaelekeza kwamba watachagua mwenyekiti miongoni mwao. Kwa hivyo, wajumbe wa Kamati Teule watakuwa ni:-

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin.
2. Mhe. Ismail Jussa Ladhu.
3. Mhe. Abdalla Juma Abdalla.
4. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa.
5. Mhe. Asha Bakar Makame.

Kamati Teule hiyo ambayo shughuli yake kubwa kama mlivyoamua Waheshimiwa Wajumbe itakuwa ni kufuatilia masuala ya Manispaa na kufuatana na kanuni vile vile tulipaswa kutoa hadidu rejea na kwa bahati nzuri hadidu hizo tumezipata kutoka kwenu Waheshimiwa Wajumbe kwa yale ambayo mliyatoa hapo kabla ilipotakiwa kamati hii ingeundwa tangu siku za kupitisha bajeti, lakini baadhi ya mengine yalipatikana katika mkutano wa juzi ambao tulikuwa tumeanza kujadili hoja ambayo iliwasilishwa na Mhe. Waziri na hatimae tukaona kwamba majadiliano yale tuyafunge na badala yake tuunde Kamati Teule kama nilivyokwishaitangaza hivi punde. Kwa hivyo, kufuatana na ripoti za *Hansard* ambazo Waheshimiwa Wajumbe mlichangia hadidu rejea za kamati hiyo zitakuwa kama ifuatavyo:

Kamati Teule iliyoundwa na Baraza kwa ajili ya kufuatilia masuala ya Baraza la Manispaa Zanzibar inapewa hadidu rejea kama hivi ifuatavyo;

1. Kuchunguza mikataba ya uwekaji mabango ya matangazo katika barabara mbali mbali iliyoingiwa baina ya Baraza la Manispaa ya Zanzibar na Makampuni mbali mbali na utekelezaji wa masharti ya mikataba hiyo. Hilo ni moja kati ya mambo ambayo mliyaeleza kwamba yana utata na yalikuwa yanahusu kufuatiliwa.
2. Kuchunguza taratibu za uidhinishaji wa matumizi na uuzaji wa rasilimali za Baraza la Manispaa Zanzibar. Hilo nalo lilikuwa ni jambo lilobishaniwa sana wakati wa majadiliano kipindi cha bajeti na yakawa yanahitaji ufafanuzi na Wajumbe walikuwa wamehitaji kuunda Kamati Teule lakini serikali ikasema itaunda kamati kufuatilia hayo na taarifa baadae ingetolewa katika Baraza hili.
3. Kuchunguza taratibu za uajiri na upandishaji vyeo katika Baraza la Manispaa na kama taratibu hizo zinazingatia sifa zinazohitajika kwa nafasi husika. Hilo nalo limeonekana katika *Hansard* katika majadiliano yaliyokuwepo wakati huo, lakini katika mjadala wa hivi karibuni imeonekana kuna tatizo ambalo linahitaji lichunguzwe nalo kama ni hadidu rejea ya nne.
4. Kuchunguza utendaji wa Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa Zanzibar juu ya tuhuma za kutofuata sheria na kanuni kwa makusudi, ubadhirifu wa fedha na kuhusika kwake katika migogoro iliyoikumba Baraza la Manispaa. Hizo ndizo hadidu rejea nne zilizokutikana katika *Hansard* ambazo wajumbe mlikuwa mnadadisi na mlikuwa mnahitaji ufafanuzi kutoka kwa waziri anayehusika na ikaonekana ufafanuzi haukupatikana sawa sawa. Kwa hivyo, naomba kuwasilisha kwenu hadidu rejea hizo ambazo zimetokana na sisi wajumbe ili zithibitishwe na hatimae ziwe ndio hadidu rejea kwa ajili ya Kamati Teule hiyo.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe naomba nitoe hoja hiyo kwenu na sasa nitake maamuzi ya Baraza hili kwa kuuliza wale ambao wanakubali hadidu hizo kama vile zilivyojitokeza katika majadiliano ya huko nyuma wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kukubaliwa)

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe Kamati Teule hiyo itapewa miongozo hii ili kuweza kuifanyia kazi za kufuatilia na kuchunguza masuala hayo. Utaratibu wa lini wataanza huo nawaachia kamati wenyewe kwa sababu najua wajumbe hawa pia ni Wajumbe wa Kamati nyengine za kudumu na zipo baadhi ya kamati ambazo tayari zilikwishakutoa ratiba zao za kazi za kamati ya kudumu. Baada ya hilo Waheshimiwa Wajumbe nakushukuruni lakini pia kuna tangazo moja kubwa muhimu.

Waheshimiwa Wajumbe mtakumbuka kwamba wakati fulani nimesahau ulikuwa ni mwezi gani lakini tulikubaliana kwamba katika maeneo ya jengo hili la Baraza maeneo ya nje yamekuwa ni maeneo ambayo yanaleta usumbufu kidogo na jua kali kutokana na kukosa miti, tukakubaliana kwamba yafaa tupande miti ili kuimarisha mazingira ya hapa pahala lakini pengine pia itasaidia kupunguza hali ya hewa katika eneo letu hili.

Kipindi ambacho tuliamua jambo hili ilikuwa ni kipindi cha mvua za Vuli ambazo zilikuwa pungufu na tukasema kwamba tusubiri Masika, ingawa Masika wenyewe nayo yanaonekana hayakuimarika vizuri lakini tunaamini bado mvua za Masika hazijaisha. Kwa hivyo, kazi hii ilikuwa ifanyike kwa mashirikiano na Wizara ya Kilimo kupitia Idara yake ya Misitu.

Waheshimiwa Wajumbe juzi kwa mashirikiano makubwa na wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo Mhe. Waziri tunamshukuru sana alinipa taarifa kazi ya kuchimba mashimo kwa ajili ya kupanda hiyo miti ilikwishafanyika na mashimo hayo ingekuwa niko shamba ningesema makoongo, lakini kwa sababu Waziri alisema kuna uchimbaji wa mashimo na mimi itabidi nitamke hivyo hivyo. Kwa hivyo, mashimo hayo yapo tayari na tumekubaliana kwamba shughuli hiyo ya upandaji miti ifanyike kesho mapema asubuhi mnamo saa 12.

Kwa hivyo, naomba Waheshimiwa Wajumbe niwaalike rasmi pengine badala ya kwenda kwenye mazoezi basi kwa kesho zoezi letu mnamo saa 12:30 asubuhi lifanyike hapa kwa kila mjumbe kupata nafasi ya kupanda mti pengine mmoja. Kila mmoja ataoneshwa shimo lake kwa ajili ya kupanda mti, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo kwa kutununulia miti hiyo ambayo itakuwa inahitajika kwa zoezi hilo tutakalofanya kesho. Kwa hivyo, kwa ujumla nimshukuru Waziri wa Kilimo mwenyewe hayupo kwa kumuamuru Katibu Mkuu wake aifanye kazi hiyo kwa ajili ya kuimarisha mazingira katika eneo letu la Baraza.

Nichukue nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe na makofi mliopiga naamini tutashiriki vizuri katika upandaji wa miti, nitamwambia Katibu atayarishe mashimo hayo kwa viongozi ili kila mmoja apate la kwake apande mti, na tuhakikishe kwamba miti hiyo hatimae tutakuwa tunailea vizuri ili kuona kwamba miti inafanikiwa. Nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe pia na Wizara ya Kilimo kupitia Idara ya Misitu kwa kushirikiana na sisi katika shughuli hiyo muhimu sana. Nakushukuruni.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya hayo sasa nichukue nafasi hii kumkaribisha Mhe. Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Makamo wa Pili wa Rais Napenda kuwashukuru na kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati hizi pamoja na Wajumbe wao, kwa kuandaa ripoti hizo nzuri zilizochunguza kwa kina mienendo ya wizara mbali mbali na taasisi zao. Ripoti hizo zimesaidia sana kuitanabahisha Serikali katika kasoro mbali mbali zilizogundulika. Serikali itazizingatia kwa makini kasoro zote zilizogundulika na kuchukuliwa hatua zifaazo kuzirekebisha au kuziondoa kabisa kasoro hizo. Na kwa kupitia Baraza hili Mhe. Spika nawaagiza Mawaziri wote kuzisimamia vyema wizara zao pamoja na Taasisi zilizo chini yao ili mapungufu hayo yasitokee tena.

Mhe. Spika, Wajumbe wako pia walipata nafasi ya kupata Taarifa ya Hoja ya Eneo la Bahari la Ukanda wa Kiuchumi iliyotolewa na Mwanasheria Mkuu; Taarifa ya Mikopo ya Elimu ya Juu iliyotolewa na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Taarifa ya Hoja ya Ripoti ya Baraza la Manispaa ya Mji wa Zanzibar iliyowasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Aidha, Baraza lako tukufu limepitisha marekebisho na mapendekezo ya kanuni za Baraza la Wawakilishi, pamoja na kujadili hoja binafsi ya Mheshimiwa Hija Hassan Hija, Mwakilishi wa Kiwani kuhusu Ripoti ya Manispaa, Baraza limeona vyema liunde Kamati Teule yake ili ikafanye uchunguzi wake badala ya kujadili ripoti ambayo siyo yake. Kuhusu hoja binafsi ya Mhe. Hija, Baraza limeamua kuwa Kamati ya PAC ikafanye uchunguzi huo.

Mhe. Spika, wakati wa kufunga Mkutano wa Sita wa Baraza lako Tukufu, nilizungumza kuhusu fedha zilizochangwa na wahisani na wananchi kwa ajili ya kuwasaidia wananchi walioathirika kutokana na ajali ya meli *M.V Spice Islander*.

Nilisema Serikali itazigawa mara moja fedha zilizopatikana kwa wananchi walioathirika na ajali hiyo baada ya kumalizika zoezi la uhakiki wa majina ya wale wote wanaostahiki kulipwa na wale wananchi wenzetu waliofariki, na wale waliookolewa wakiwa hai. Napenda kuliarifu Baraza lako tukufu na wananchi wote kuwa, Serikali tayari imeshaanza ugawaji wa fedha hizo kwa kisiwa cha Unguja na linaendelea vizuri. Hadi kufikia tarehe 17 Aprili, 2012 kati ya watu 457 waliofariki watu 256 sawa na asilimia 57 tayari wameshapatiwa fedha zao. Aidha, jumla ya watu 122 waliookolewa sawa na asilimia 63 wameshalipwa fedha zao kati ya watu 193. Na wale ambao walihusika katika ajali ile na majina yao hayajajitokeza katika orodha ya malipo, Serikali itayafanyia tathmini na wale wote waliohusika Serikali itawapatia haki zao. Baada ya kumalizika kwa zoezi hili hapa Unguja, zoezi litaanza rasmi kwa upande wa Pemba, nalo litafanyika baada ya muda mfupi.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena, nachukua fursa hii adhimu kuwapongeza sana wananchi kwa ustahamilivu na uvumilivu wao, ambao umetusaidia sana kuendesha zoezi hili la uhakiki wa majina hadi kufikia hatua ambayo sasa tunalipa fedha tulizoahidi kwenye Baraza hili. Tunatoa wito pia kwa wananchi wote, kufika katika vituo walivyopangiwa kwa kufuata utaratibu unaoendelea kutolewa kupitia vyombo vya habari hasa Shirika la Utangazaji la Zanzibar kupitia radio yake.

Mhe. Spika, utekelezaji wa bajeti katika kipindi cha mwezi Julai hadi Februari 2011/2012 ni wa kuridhisha, ingawa bado tumeendelea kuwa na changamoto katika upatikanaji wa rasilimali kutoka nje kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo. Katika kipindi hicho jumla ya Shilingi 340,969 milioni zimekusanywa sawa na asilimia 55.6 ya makadirio ya mwaka ya Tsh. 613,076 milioni. Aidha jumla ya matumizi katika kipindi hicho yamefikia Tsh. 296,766 milioni sawa na asilimia 69 ya makadirio ya mwaka.

Mhe. Spika, zao la karafuu ni zao mama hapa kwetu Visiwani, na litaendelea kuwa tegemeo la uchumi wetu kwa miaka mingi ijayo. Kwa bahati mbaya zao hili linakabiliwa na tatizo la ukongwe wa mikarafuu, unaopelekea uzalishaji mdogo wa zao hili. Katika kutimiza azma ya kuimarisha zao la karafuu ili kuongeza uzalishaji, na hatimaye kuongeza kipato cha wananchi na Taifa kwa jumla, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili, inaendelea na kampeni ya upandaji mikarafuu katika maeneo yote husika, ili kuutumia vyema msimu wa mvua zinazoendelea.

Wizara ya Kilimo na Maliasili kupitia Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka, imejiandaa kuhakikisha miche ya kutosha inapatikana katika vitalu vyake na kwamba wakulima wote nchini watapatiwa miche hiyo bila ya malipo. Nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu wanaotoka maeneo yanayolimwa karafuu kuichangamkia miche inayotolewa, kwa kuwahamasisha wananchi katika majimbo yao kuipanda miche hiyo kwa wingi. Tunawaomba wakulima na wananchi wote kwa jumla, kuitumia fursa hii adhimu kuzingatia maelekezo na masharti ya msingi yanayotolewa na wataalamu, ikiwemo utayarishaji wa mashamba kabla ya kupatiwa miche hiyo.

Mhe. Spika, kilimo cha Mpunga nacho kinaendelea vizuri msimu huu ikilinganishwa na msimu uliopita licha ya matatizo yaliyojitokeza ambayo yametokana na mabadiliko ya hali ya hewa. Takwimu zilizokusanywa na Wizara ya Kilimo na Maliasili zinaonesha kwamba jumla ya eka 28,400, sawa na asilimia thamanini na mbili (82%) ya lengo lililowekwa zimelimwa Unguja na Pemba hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2012 na kazi bado inaendelea. Hata hivyo, upatikanaji wa ruzuku ya pembejeo na huduma za utayarishaji wa mashamba haukuweza kuwafikia wakulima wote kama tulivyotarajia, kutokana na kuwepo kwa idadi kubwa ya wakulima waliohamasika, na kujitokeza kutumia huduma hizo ukilinganisha na uwezo uliokuwepo.

Serikali itaendelea kufikisha huduma hizo kwa wakulima wengi kadri itakavyowezekana katika misimu ijayo, ili waweze kuongeza uzalishaji na hatimae kujiongezea chakula na kipato chao na taifa kwa jumla. Aidha, Serikali inawaomba wakulima kuzingatia ushauri unaotolewa mara kwa mara na wataalamu wetu wa kilimo kupitia vyombo vya habari, ikiwemo matumizi ya mbegu bora, na kulima kwa kuzingatia mabadiliko ya miongo ya mvua, ili waweze kuepuka hasara zilizojitokeza katika baadhi ya maeneo msimu uliopita.

Mhe. Spika, sekta ya mawasiliano ni muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu. Mipango ya Serikali yetu ya kuunganisha miji na vijiji kwa mtandao wa barabara itaendelea kutekelezwa kwa kasi zaidi Unguja na Pemba. Katika kikao kilichopita cha Baraza letu nilizungumzia barabara ya Mfenesini - Bumbwini yenye urefu wa kilomita 13.2 kuwa iko katika hatua za kukamilika. Napenda kulijulisha Baraza lako Tukufu kuwa barabara hii imekamilika sasa, pamoja na madaraja ya Mwanakombo, Tingatinga na Mto wa Maji. Kukamilika kwa barabara hii pamoja na madaraja niliyoyataja, kunategemewa kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi ikiwemo usafirishaji wa bidhaa kwenda kwenye masoko kwa urahisi zaidi, pamoja na kufungua maeneo yetu kwa wawekezaji wa ndani na nje.

Nawaomba wananchi wanaoishi sehemu ambazo madaraja hayo yamejengwa kuwa walinzi dhidi ya uharibifu wa aina yoyote ile, ili yaendelee kutuhudumia kwa miaka mingi ijayo kama tulivyokusudia. Aidha, nawaomba madereva wanaotumia madaraja haya kuwa waangalifu, kwani uzoefu wetu unaonesha kuwa ajali nyingi za barabarani Mkoa wa Kaskazini, hutokea mara kwa mara sehemu zenye madaraja. Nawaomba sana wadereva hao waepuke ajali hizo kwa kufuata sheria za barabarani.

Mhe. Spika, Serikali yetu kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo hivi karibuni imekarabati mtambo wa mawimbi mafupi (*short waves*) uliopo Dole kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa

China. Mtambo huo umekabidhiwa kwa Serikali tarehe 9 Machi, 2012. Kukarabatiwa kwa mtambo huo, kunafanya matangazo ya redio ya Shirika la Utangazaji (*ZBC*) kusikika hadi nchi za Mashariki ya Kati.

Wizara pia inaendelea na ujenzi wa studio na ofisi katika eneo la Bungi, pamoja na nyumba mbili za kisasa za wafanyakazi zinazojengwa kwa lengo la kuimarisha utendaji mzuri wa kazi. Studio imehamishiwa Bungi kutoka Chumbuni, kwa sababu za usalama wa ndege uliokuwa ukihatarishwa na mnara uliokuwepo huko.

Mhe. Spika, sekta ya Utalii itaendelea kuwa tegemeo la uchumi wa nchi yetu, na ndio maana Serikali yetu kila inapoona kuna haja ya kujenga mazingira mazuri kwa lengo la kuimarisha sekta hiyo huwa inafanya hivyo. Marekebisho ya Sheria namba 6 ya Mwaka 2009 na Mswaada wake kupitishwa na Wajumbe wa Baraza lako Tukufu katika mkutano huu, ni hatua muhimu kuelekea kwenye utalii utakaosaidia juhudi zetu za kujenga maisha mazuri kwa wananchi wetu. Kamisheni yetu ya Utalii katika jitihada zake za kuimarisha Utalii nchini kwa njia ya kuitangaza Zanzibar katika nchi mbali mbali duniani imepata mafanikio mazuri.

Hivi karibuni Zanzibar imepata tunzo ijulikanayo "*The Annual Russian Tourism Award"* kwa kuwa kituo bora cha utalii barani Afrika. Tunaipongeza Kamisheni yetu ya Utalii kwa mafanikio haya makubwa, na tunawaomba waendelee na jitihada zao za kuitangaza Zanzibar duniani kote. Hata hivyo, ni vyema ikafahamika kuwa kazi ya kuitangaza Zanzibar ni kazi yetu sote. Wengi wetu Barazani hapa tunapata fursa ya kutembelea nchi tofauti duniani. Tutumie basi fursa kama hizo kuitangaza nchi yetu kwa watu tunaokutana nao.

Mhe. Spika, Taifa letu linatambua haki za walemavu. Watu wenye ulemavu wana haki na fursa sawa kwa wote. Si vyema kwa jamii yetu kuendelea na tabia ya kuwanyanyasa na kuwadhalilisha watu wenye ulemavu. Taasisi nyingi za Serikali hivi sasa zinajenga majengo mapya. Natoa wito kwa wale wote wanaojenga majengo kwa ajili ya kutoa huduma za umma, kuhakikisha kwamba majengo hayo yanakuwa rafiki kwa watu wenye ulemavu. Kuwa rafiki maana yake mlemavu aweze kutumia jengo hilo kama watu wengine, kwa kuwekewa miundombinu ambayo itamrahisishia kuingia ndani ya jengo hilo, na kutumia fursa zilizomo ndani yake.

Kwa mfano, majengo hayo yanatakiwa kuweka vyoo maalum kwa ajili ya watu wenye ulemavu katika ghorofa zote za jengo, na pia mlemavu apate fursa ya kwenda ofisi yoyote ndani ya jengo hilo bila ya vikwazo. Suala la ajira kwa watu wenye ulemavu wenye sifa na uwezo ni la umuhimu pia. Waajiri wasiwanyime fursa watu hawa kwa sababu tu ya ulemavu wao, ni muhimu kuangalia sifa na uwezo wao na kuwapa vipaumbele. Ubaguzi mzuri *(Positive discrimination)* wakati mwengine inafaa kutumika katika jamii, kwa lengo la kuwanyanyua wale walioachwa nyuma. Kwa hivyo suala la kuwapa vipaumbele walemavu wakati wa ajira ni muhimu sana.

Mhe. Spika, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imetayarisha Sera ya Mifugo ambayo imeweka mazingira mazuri na mikakati endelevu ya kuendeleza sekta ya mifugo. Sera ya sasa imezingatia mambo muhimu ya kuiendeleza sekta hiyo ambayo hayakuwemo katika sera iliyokuwepo. Mambo yaliyokuwemo katika sera ya sasa ni pamoja na mambo ya utafiti, ustawi wa wanyama, uzalishaji na utumiaji wa nishati itokanayo na samadi, kuongeza thamani ya mazao yatokanayo na mifugo, kuendeleza uzalishaji wa ndani na upatikanaji mitaji ya fedha kwa wajasiriamali. Sera hii tunategemea itakuwa kichocheo cha ufugaji bora nchini.

Mhe. Spika, nchi yetu ilikumbwa na uhaba wa mchele wiki za mwanzo wa mwezi wa Machi, 2012, hali ambayo ilisababisha bei ya mchele kupanda kutoka shilingi 50,000/= kwa kipolo cha kilo 50 mpaka shilingi 57,000/=. Hali hii ilisababishwa na kuchelewa kufika kwa mchele ulioagizwa mwishoni mwa mwezi wa Machi, 2012. Hata hivyo, tayari mchele umeanza kuingia kutoka nje ambapo kiasi cha tani 12,251 zimeingia mapema mwezi huu. Mchele huo unatarajiwa kutumika kwa miezi miwili, matumizi kwa mwezi yanakisiwa kuwa ni tani 6,000. Kwa upande wa bei hivi sasa imeshuka, na mchele unapatikana kwa shilingi 52,000/= kwa kipolo cha kilo 50. Tunawasihi wafanya biashara kuacha tabia ya kuutorosha mchele wetu kimagendo kwa sababu ya kushuka kwake bei.

Mhe. Spika, Serikali kupitia Wizara ya Afya inatarajia kuanzisha kampeni ya Kitaifa ya kutoa dawa za Kichocho na Minyoo kwa Wananchi kuanzia tarehe 28 mwezi huu wa Aprili. Madhumuni ya kampeni hii ni kupambana na maradhi ya Kichocho na Minyoo ambayo yamekuwa yakisumbua Wananchi wengi, hasa watoto katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa taarifa za kitaalamu, maradhi ya kichocho yameenea kwa asilimia 15 kwa kisiwa cha Pemba na asilimia 8 kwa kisiwa cha Unguja. Hii ina maana maradhi ya kichocho yapo katika Visiwa vyetu

vya Unguja na Pemba. Na kwa Unguja maradhi yamesambaa zaidi katika Mkoa wa Kaskazini. Serikali kupitia Wizara ya Afya imekuwa ikichukua jitihada mbali mbali kutokomeza kichocho na minyoo, ambapo kampeni hii ni mojawapo ya juhudi hizo.

Mhe. Spika, dawa hizi ni za kuzuia wadudu wa kichocho na kuua minyoo iliyokuwemo mwilini, Dawa hizi hazina matatizo kwa afya ya binaadamu na Serikali imeamua kuzitoa dawa hizi bure. Hivyo natoa wito kwa wananchi wote kutokua na khofu juu ya madhara ya dawa hizi. Nawaomba Wawakilishi wenzangu kushajiisha na kuwaelimisha wananchi kula dawa. Narejea tena dawa hizi hazina matatizo kwa afya ya binaadamu, tuzitumieni ili lengo la Serikali yetu la kutokomeza kabisa kichocho nchini ifikapo 2015 lifanikiwe.

Mhe. Spika, kama tujuavyo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimo katika maandalizi ya Sensa ya Watu na Makaazi, ambayo imepangwa kufanyika nchini kote kuanzia Jumapili ya tarehe 26 Agosti mwaka huu, Taarifa zitakazokusanywa katika Sensa ya mwaka 2012 zitatumika kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2020 kwa Zanzibar, Mkakati wa Kukuza na Kupunguza Umaskini Zanzibar - MKUZA. Takwimu hizo zitatumika pia kutathmini utekelezaji wa malengo ya Milenia ifikapo mwaka 2015.

Mhe. Spika, kauli mbiu ya Sensa ya safari hii ni **"Sensa kwa Maendeleo ya Taifa: Jiandae kuhesabiwa".** Kauli mbiu hii tuifanyie kazi sote kwa pamoja, Viongozi na wananchi tunaowaongoza katika kufanikisha sensa ya safari hii. Maelezo mengi yametolewa kuhusu umuhimu wa sensa kwa maendeleo yetu. Kwa kifupi sensa inatueleza sisi ni nani na kwa namna gani tumebadilika kwa kipindi kilichopita. Takwimu za sensa zinasaidia sana Serikali kupanga mipango yake kwa kufahamu vyema mahitaji ya wananchi wake. Takwimu hizi pia zitatusaidia katika kushajiisha uwekezaji katika nchi yetu. Takwimu sahihi za idadi ya watu, hali ya uchumi wa nchi kwa jumla ni miongoni mwa taarifa muhimu kwa muwekezaji.

Kwa rafiki zangu wafanyabiashara, takwimu za sensa zitawasaidia wapi katika nchi wafungue biashara zao. Sisi Wanasiasa pia takwimu hizi za sensa zitatusaidia kujua wapiga kura wengi tutawapata vijiji vipi! Takwimu za sensa tutakazozipata baada ya sensa hii ni mali kwa kila mwananchi, inategemea tutazitumia vipi. Maelezo mengi kuhusu Sensa hii tumeshayapata kupitia Semina mbili tulizofanyiwa na Wataalamu wetu wa Sensa. Ni matumaini yangu kwamba yale yote tuliyoelezwa katika semina hizo tutayafanyia kazi ipasavyo.

Mhe. Spika, jukumu la kila Kiongozi kuanzia chini hadi juu kuelekeza uongozi wake wa busara katika kufanikisha sensa ya mwaka huu, na jukumu la mwananchi kuanzia sasa kuhakikisha kuwa siku ya Sensa inapowadia anakuwa mstari wa mbele katika kuhesabiwa. Natoa wito kwa kampuni mbali mbali nchini zijitokeze kusaidia kuhamasisha sensa ya mwaka huu. Milango iko wazi kampuni hizo kushirikiana na Kamati ya Taifa ya Sensa katika kuhamasisha wananchi kwa vipeperushi au hata kuchapisha fulana na mambo kama hayo.

Mhe. Spika, sote ni mashahidi, nchi yetu iko katika hali ya kupigiwa mfano wa Amani na Utulivu na hasa baada ya Kuundwa kwa Serikali ya Mapinduzi yenye Mfumo wa Umoja wa Kitaifa. Matumaini ya wananchi wetu, hali hii itabakia na itaendelea kwa kizazi kilichopo na kijacho.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kwa upande wake imedhamiria kwa dhati kudumisha hali hii ya amani na utulivu Visiwani mwetu. Kurasa zetu za historia ambazo zilijaa migogoro ya kisiasa, uhasama na hali ya kutoaminiana, tumezitia moto; kurasa tulizonazo tunaandikia historia yetu mpya, kichwa chake cha habari kinasomeka; Umoja, Amani na Utulivu. Ndani ya kurasa hizo habari tunazozinakili na ambazo zimetawala ni maendeleo kwa wote; haki kwa wote; maji safi kwa wote; elimu bora kwa wote, afya njema kwa wote na kadhalika. Hakuna mwenye ubavu kubadilisha kichwa hichi cha habari, kwani wenyewe tupo macho. Pia hakuna mwenye ubavu kubadilisha yale tunayoyanakili kwenye kurasa hizi, kwani wenyewe tupo kuangalia.

Mhe. Spika, hivi karibuni kumetokea kikundi cha wenzetu wachache kinachoendesha makongamano na mihadhara inayotishia hali yetu ya **amani na utulivu** niliyoielezea. Kikundi hichi mbali na kuhamasisha kwa nguvu watu kuukataa Muungano, pia kinatukana kwa nguvu Viongozi wetu na wale wanaounga mkono Muungano.

Mhe. Spika, Serikali haikatazi kikundi chochote kuendesha mihadhara au makongamano nchini, na ndio maana tumevumilia tukidhani kuwa nia ya mihadhara hiyo ni kuelimisha jamii, lakini mihadhara hiyo imebadilika sura na badala ya kuelimisha imekuwa ni uwanja wa kashfa, kejeli na matusi tena matusi mengine ni ya nguoni kwa Viongozi wetu, jambo ambalo ni kinyume kabisa na utamaduni wa mzanzibari na misingi ya kidemokrasia.

Mhe. Spika, napenda ifahamike wazi kuwa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haitakivumilia kikundi chochote kitakachoonekana kuhatarisha amani, utulivu na umoja wa wananchi wetu. Hatuko tayari kurudishwa kule tulikotoka ambako tukiishi kwa chuki na uhasama mkubwa. Hatutasita kukizuia kikundi chochote kile kuendesha mihadhara au makongamano tutakayobaini yanahatarisha usalama wa nchi yetu. Kwa hili hatutokuwa na muhali na mtu yoyote yule.

Mhe. Spika, ninawaomba sana Watanzania wenzangu kuwa fursa iliyotolewa na Serikali zetu kwa kuleta mchakato wa katiba mpya ni jambo la kihistoria, na linaloonesha kukuwa kwa demokrasia katika nchi yetu. Hivyo litakuwa ni jambo la busara sana kutumia fursa hii kwa mustakabali wa nchi yetu, badala ya baadhi ya wenzetu kujitokeza kuharibu dhamira njema ya Serikali.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena napenda kukushukuru wewe binafsi na kwa kupitia kwako kwa Naibu Spika na Wenyeviti wetu wa Baraza la Wawakilishi, kwa namna mlivyouendesha mkutano huu kwa busara na utulivu mkubwa. Mkutano huu ulijaa hekima, maarifa na uvumilivu mkubwa. Hivyo, napenda niwapongeze Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza kwa michango yao mizuri, iliyokuwa ya faida kubwa kwa Serikali. Hii imeonesha uwezo wao wa kuisimamia na kuielekeza Serikali vizuri. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeithamini sana michango hiyo, na naahidi Serikali itachukua hatua kwa yale yote ambayo Wajumbe wameyaelekeza.

Mhe. Spika, kuhusu taarifa ya Kamati Teule ambayo imewasilishwa katika Baraza lako Tukufu na kuchangiwa na Waheshimiwa Wajumbe kadhaa wa Baraza lako tukufu. Kwa niaba ya Serikali, nachukua fursa hii kuipongeza sana kazi iliyofanywa na Kamati hiyo pamoja na michango yote iliyotolewa kuhusiana na ripoti hii.

Ripoti ya Kamati Teule imetupa nafasi nyengine kama Serikali, kuona namna ambavyo Baraza la Wawakilishi katika Awamu ya Saba ya Serikali ya Zanzibar, limejipanga kuona kuwa Serikali inabadilika katika utendaji wake na uwajibikaji wake.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inathamini juhudi hizi za Baraza la Wawakilishi, kwa sababu zimeunga mkono kauli mbiu ya Serikali ya Awamu ya Saba kuwa tunaachana na utendaji wa kimazoea *(Business as usual).*

Mhe. Spika, mara zote Mhe. Rais wa Zanzibar anakuwa akisema “Tushirikiane kupambana na rushwa, wizi na ubadhirifu wa mali ya umma kwa lengo la kujenga Taifa lenye kufuata Utawala Bora, usawa na haki za Binadamu”. Lazima sote ndani ya Serikali tuuheshimu msemo huu wa Rais wetu.

Mhe. Spika, Serikali inachukulia taarifa ya Kamati Teule (miongoni mwa Kamati nyengine za Baraza), kuwa ni mchango thabiti wa Baraza katika kuunga mkono juhudi na mwelekeo wa Serikali ya Zanzibar ya Awamu hii. Serikali kuu imetoa mwelekeo, Baraza la Wawakilishi limetoa mfano mzuri juu ya mwelekeo huo. Sasa ni jukumu la Watendaji wa Serikali katika ngazi zote kufuata nyayo, na tunakiri kuwa ni jukumu la Uongozi wa juu wa Serikali kulisimamia jambo hili.

Mhe. Spika, Serikali imeyasikia vizuri maelezo yaliyomo kwenye taarifa ya Kamati, pamoja na michango mizuri ya Wajumbe wa Baraza. Nataka kulihakikishia Baraza lako Tukufu kwamba, Serikali nayo itakuwa makini sana katika kuifanyia kazi kwa vitendo taarifa ya Kamati Teule. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mwisho kabisa nawatakia Wajumbe wote safari njema ya kurejea Majimboni mwao, ili wakaungane na wananchi wao kuendeleza harakati zao za kuyaletea Majimbo yao maendeleo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kutoa hoja ya kuliakhirisha Baraza lako Tukufu hadi Jumatano tarehe 13 Juni, 2012 saa 3:00 asubuhi.

Mhe. Spika**,** naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Makamo wa Pili wa Rais nami nichukue nafasi hii, kwa niaba ya waheshimiwa wajumbe kukushukuru sana kwa hotuba hiyo ya ufungaji wa mkutano huu wa saba, hotuba imetoa mwelekeo mzuri, na imeonesha wazi msimamo wa serikali juu ya shughuli za baraza hili, na kwa pamoja kufanya kazi kwa mashirikiano kati ya wawakilishi, wananchi, pamoja na serikali kwa manufaa ya wananchi wetu. Sina budi kukushukuru sana wewe binafsi, pamoja na waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri pamoja na Waheshimiwa wajumbe wote kwa mashirikiano makubwa ya kuendesha shughuli zetu hapa barazani hasa katika mkutano huu ambao kihistoria ni mkutano mfupi, lakini umekuwa mrefu kwa mwaka huu.

Tayari shughuli ambazo tumezipitisha hapa umezisema, sina haja ya kuzieleza tena, lakini nichukue nafasi hii vile vile kwamba kazi hiyo nzuri ya mkutano huu wa saba isingefanikiwa kama sio kwa mashirikiano makubwa sana ya watendaji wangu, ambao mara zote wamekuwa wanajitahidi ili kuwahudumia waheshimiwa wajumbe, kuweza kumudu kufanya shughuli zetu hapa kwa ufanisi mkubwa.

Kwa hivyo niwashukuru kupitia kwa katibu, watendaji wote wa baraza kwa kufanikisha shughuli za mkutano huu kama ilivyo kawaida yao, lakini bila ya kusahau waandishi wa habari na hasa wachukuaji wa maelezo ya baraza hapa *camera man* waliopo kwa kazi nzuri sana, ambayo muda wote huwa naona ndugu zetu hawa wapo, kimsingi sura ndio hizi hizi zinazokuwepo, wanakuwepo muda wote bila ya kuchelewa na kuona kwamba shughuli hizi zinaoneshwa *live* kwa wananchi wetu na pia ndani kuweza kuona. Mashirikiano makubwa hayo ndiyo yaliyofanya shughuli zetu kwa mkutano huu wa saba kufanikiwa vya kutosha kiasi hicho nawashukuru sana.

Waheshimiwa wajumbe baada ya shukurani hizo, sasa naomba niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, kuakhirisha mkutano huu wa saba hadi tarehe 13 siku ya Jumatano Juni mwaka huu Saa 3.00 za asubuhi wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 12.03 Jioni Baraza liliakhirishwa hadi
Jumatano tarehe 13/06/2012 Saa 3.00 Asubuhi)